# Nipashe

Ijumaa Machi 20, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580184

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Abambwa na magunia ya kondomu akidai amegawiwa kwenye semina

UKURASA 12


BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Daraja Namba sita Afrika linalotarajiwa kuleta uchumi, maisha mpya Kanda ya Ziwa
Ewura walivyopania mwisho wa 'vishoka' umeme Nyanda za Juu
UCHUMI
Habari katika picha
Vita vya corona: Njia 5 kufanya kazi nyumbani Ukurasa 15

UKURASA 13

TISHIO LA CORONA

# Mchungaji akemea wanaofanya mizaha



**BAA LA CORONA**

**Wataalam wa afya wanashauri kama mtu ana homa au kukohoa mara kwa mara, anatakiwa kubaki nyumbani kwa saa saba, na watu wanaoishi naye wanatakiwa wabaki nyumbani kwa siku 14 waletewe chakula au dawa nyumbani. BBC**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sababu na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana na kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa ziba mdomo**

• **Ataka** waheshimu maelekezo ya wataalamu, Magereza yapiga 'stop' vyakula mahabusi, kanisa latenga siku ya maombi, ratiba Kidato cha 6 yabadilishwa...

*Habari 2,3,8,26*



Mchungaji Dk. Eliona Kimaro. **PICHA: MAKTABA**

## Mwalimu anusurika kuuawa na wananchi

UKURASA 4




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store




## Membe akoleza moto tume huru uchaguzi

UKURASA 4


**MICHEZO** **SIMBA, YANGA ZAIGOMEA TFF** UK.32 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kamati zote Bunge zarudishwa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameagiza Kamati za Bunge za kisekta zilizoko kwenye ziara ya kukagua miradi kwenye mikoa mbalimbali nchini, kurejea mara moja Dodoma kutokana na tishio la ugonjwa wa Corona.

Aidha, Bunge limesitisha utaratibu wa kupokea wageni mbalimbali wakiwamo wanafunzi kwa lengo la kujifunza shughuli za chombo hicho.

Sambamba na hilo, Kituo cha Afya cha Bunge kimeanza kutengeneza maji ya kunawia mikono kwa kuongeza kiwango cha chlorine (water sanitizer) ambayo inakubalika na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Shirika la Afya Duniani(WHO).

Ndugai alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa akibainisha hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa na serikali.

"Kamati zetu za kisekta zilikuwa katika ziara ya kukagua miradi mbalimbali kuangalia utekelezaji, ambayo ilipangiwa fedha kwa mwaka unaoishia Juni, mwaka huu. Tumechukua hatua kuzielekeza popote zilipo kurudi Dodoma mara moja," alisema.

Ndugai alisema kazi ya uchambuzi wa bajeti itakayofanywa na kamati itafanyika Dodoma katika maeneo ya majengo Bunge kwa zamu.

"Kwenye maeneo yetu ya bunge tumechukua hatua mbalimbali ikiwamo kuwasisitiza wabunge kunawa mikono mara kwa mara na kutumia vitakasa mikono, vilivyopo kwenye mageti na pia tumeweka vipima joto vinavyotambua dalili za awali za Corona,"alisema.

Alishauri wabunge watakapokuwa Dodoma kujizuia kujichanganya kwenye makundi mbalimbali huku akisema liko hema maalum pembezoni kwa ajili ya atakayeshukiwa kuwa na virusi vya Corona.

"Kamati zikiwa hapa tutazipanga. Kuna baadhi zitakuja asubuhi na zingine mchana kuelekea jioni. Kazi nyingi sana za kamati tutazifanya kwa kupitia njia ya mtandao kwa kutumia 'tablets' ambazo wanazo, itakuwa kidijitali zaidi," alisema.

Kuhusu wageni, Spika alisema watakaoruhusiwa kuingia bungeni ni wale wenye kazi na vibali maalum tu.

"Hivyo tunaomba wadau mbalimbali kusitisha maombi ya kutembelea Bunge hadi hapo itakapoelekezwa vinginevyo,"alisema.

Akizungumzia kuhusu maji yanayotengenezwa na kituo cha Afya Bunge, Spika Ndugai alisema maji hayo yatasaidia endapo kukiwa na uhaba wa Sanitizer kwenye bunge hilo.

Alisisitiza kuwa Machi 31, mwaka huu kabla ya bunge kuanza vikao vyake atatoa utaratibu mwingine utakaotumika ili kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo bila kuathiri bajeti ya serikali ya mwaka ujao wa fedha 2020/21 itakayoanza kutumika Julai Mosi, mwaka huu.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu tahadhari zilizochukuliwa na Bunge kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mchungaji akemea mizaha kuhusu corona

**Na Romana Mallya**

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, amewakemea watu wanaofanya mzaha kuhusu virusi vya corona, ikiwamo kusingizia damu ya Yesu.

Amewataka waumini na Watanzania kwa ujumla kutopuuza maelekezo na tahadhari zinazotolewa na serikali kuhusu ugonjwa huo licha ya kwamba wanasali na kuomba.

Mchungaji Kimaro aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa ibada ya asubuhi ambayo alitumia nafasi hiyo kuwaambia waumini na Watanzania kuwa wachukue tahadhari kwa ajili ya afya zao.

"Ijumaa iliyopita tulikuwa na maombi si ya taifa bali dunia nzima ya kuiombea dunia kuhusu janga na mtikisiko wa virusi vya corona. Mpaka sasa hakujaripotiwa vifo Tanzania zaidi ya kesi chache katika baadhi ya mikoa. "Tunashukuru serikali na viongozi wake kwa namna ambavyo wanachukua tahadhari kwa ajili ya afya zetu. Tunashukuru kwa uongozi na maelekezo yanayoendelea kutolewa.

"Mliopo hapa na wengine kutoka mataifa mbalimbali mnaotusikia ninawaomba sana mzingatie maelekezo. Ninajua tunaamini na tunaomba na mimi ni mwombaji hata hizi dakika chache zilizopita nimeomba na Ijumaa iliyopita tumeomba.

"Ninasema waziwazi kwamba tunapoomba lazima tuiishi imani. Pamoja na imani tulio nayo ya maombi, ni lazima tuchukue tahadhari za msingi ambazo tumepewa, kwanza kuepuka makusanyiko yasiyokuwa ya lazima," alisema.

Mchungaji Kimaro alisema wakati huu ambao watoto wako nyumbani baada ya serikali kufunga shule, wasiruhusiwe kuzurura mtaani.

"Wasianze misele (kuzurura) wakae nyumbani baba, mama au mlezi hakikisha wanakaa nyumbani si kuzurura barabarani. Kama serikali imewarudisha nyumbani basi chukueni tahadhari.

"Dunia inamtikisiko mkubwa usifikiri kusimamisha masomo. Dunia imesimama, Marekani, Ulaya, hapa kwetu kuna mkutano wa SADC (Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika) ulikuwa ufanyike, lakini unafanyika kwenye mtandao," alisema.

Mchungaji Kimaro alisema hata Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, amehutubia na kuongoza misa kupitia mtandao kutokana na janga hilo la corona.

"Mataifa yamesimama, ndege zimezima injini zao. Ni mtikisiko mkubwa sana wa kiuchumi duniani. Hili suala ni anguko la kiuchumi duniani. Tahadhari zitatusaidia wakati mwingine kuondokana na tatizo hili," alisema.

Alisema wameona taifa lililoshambuliwa zaidi duniani ni Italia ambako ni makao makuu ya Kanisa Katoliki na kueleza kuwa hakuna Mkatoliki kuliko Papa, yeye ndiye mkatoliki wa mwisho.

"Ikiwa ndugu zetu imefika mahali wakazingatia masharti ya kiafya pamoja na imani na maombi ninaomba tusifanye ubishi. Ninaona kwenye mitandao ya kijamii vinatembea vitu kuwa usinawe tumia damu ya Yesu. Wewe ukome, damu ya Yesu ipo na kemikali ya kunawa mikono ipo," alikemea. Mchungaji Kimaro aliwataka watu wanaopotosha kwenye mitandao wasilete imani za ukichaa au uwendawazimu.

"Hapa kanisani tunazo kemikali za kunawa mikono za vimiminika kila mlango. Ukiingia kwenye ibada hii hakikisha unanawa mikono. Nyumbani tumia hizo kemikali na kama huna tumia sabuni, lakini isiwe ya kipande na unawe na maji yanayomiminika," alielimisha.

# Wagonjwa wengine 2 wagundulika Dar

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya wagonjwa waliobainika kuwa na maambukizo ya virusi vya corona nchini imefika sita baada ya jana kugundulika kwa wagonjwa wengine wapya wawili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wagonjwa wapya wawili walithibitishwa kuwapo jijini Dar es Salaam.

Alisema mmoja wa wagonjwa hao ni Mtanzania, mwanaume (40) aliyesafiri nchi za Uswisi, Denmark na Ufaransa kati ya Machi 5 hadi 13 mwaka huu na kurudi nchini Machi 14 mwaka huu.

Alimtaja mwingine kuwa ni Mtanzania mwanaume (40) aliyekuwa Afrika Kusini kati ya Machi 14 na 16 mwaka huu na kurejea nchini usiku wa Machi 17 mwaka huu.

"Wahusika wote wametengwa na hali zao zinaendelea vizuri. Juhudi za kufuatilia watu waliokuwa karibu na wagonjwa waliothibitika kuwa na virusi vya corona zinaendelea," Waziri Mwalimu alisema katika taarifa yake hiyo.

Hata hivyo, hadi juzi, idadi ya wagonjwa waliokuwa wametangazwa na serikali kupitia kwa waziri huyo ilikuwa watatu, hivyo ongezeko la jana lilimaanisha nchi kuwa na wagonjwa watano, lakini taarifa ya jana ya wizara ilibainisha kuwa idadi ya wagonjwa ni sita.

Nipashe ilipowatafuta maofisa kutoka Kitengo cha Mawasiliano ya Wizara ya Afya jana, kupata ufafanuzi kuhusu utata uliojitokeza katika idadi ya wagonjwa, ilijibiwa kuwa idadi ya wagonjwa ni sita na ufafanuzi utatolewa baadaye.

Taarifa hiyo ya wizara ilibainisha kuwa hadi jana, watu 46 wanafuatiliwa jijini Arusha na watu 66 wanafuatiliwa jijini Dar es Salaam.

## TISHIO CORONA




Askari wa kampuni ya ulinzi ya Night Support, Hashim Majito, akimnyunyizia dawa (sanitizer) ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, mmoja wa wafanyakazi wa kampuni ya The Guardian Ltd inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# ‘Marufuku chakula mahabusi gerezani’

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limezuia upelekaji wa chakula kwenye magereza wala huduma yoyote kwa mahabusi badala yake huduma hiyo itafanywa na jeshi hilo kutokana na tishio la ugonjwa wa corona.

Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi hilo, Amina Kavirondo, alitangaza zuio hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa huo jijini hapa.

Alisema jeshi hilo limesitisha kila kitu baina ya mahabusi na raia wa nje na wameweka dawa za kujikinga kwa askari magereza na wafungwa.

“Hakutakuwa na ruhusa ya mtu yeyote kuleta chakula kwa mahabusi, shughuli hiyo itafanywa na Jeshi la Magereza,” alisema.

Kavirondo alisema jeshi hilo litaendelea kuchukua tahadhari na hatua kwa kadri litakavyoona inafaa sambamba na kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali dhidi ya ugonjwa huo.

# BoT yawaondoa hofu wananchi kupata corona kwa kushika noti

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imewaondoa hofu Watanzania juu ya kupata ugonjwa wa corona kwa kushika fedha za noti kwa kuwa zimetengenezwa kwa namna ambayo inazuia vimelea vya wadudu wa aina yoyote kusalia kwenye noti hizo.

Mkurugenzi wa Huduma za Kibenki wa BoT, Augustine Hotay, alisema jana alipowasiliana na waandishi wa habari kupitia barua pepe kuwa kutokana na hali hiyo, watu wanapaswa kuondoa hofu.

“Hata hivyo, kwa kuwa noti hizi zinapita katika mikono mingi, tunawashauri wananchi kuzingatia miongozo mbalimbali inayotolewa na mamlaka zenye dhamana ya afya ya jamii, ikiwa ni pamoja na kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia maji yanayotiririka na sabuni au kutumia vitakasa mikono (sanitizers),” alisema.

Hotay alisema kwa kufanya hivyo, kutasaidia kuua vimelea kwenye mikono na kujihakikishia usalama zaidi.

Aidha, aliwashauri wananchi kufanya miamala kwa kutumia njia mbadala za malipo kama vile simu za mkononi, intaneti na kadi, bila kulazimika kufika kwenye kaunta za benki au mashine za kutolea fedha (ATM) kuchukua noti. Hotay aliwasihi wananchi katika kipindi ambacho taifa liko katika mapambano dhidi ya COVID-19, kuzipuuza taarifa zinazozagaa mitandaoni ambazo hazina vyanzo vya uhakika, zinazozihusisha fedha za noti na usambaaji wa virusi vya corona.

Shirika la Afya Duniani (WHO), hivi karibuni lilitangaza ugonjwa wa corona ni tishio duniani kote na tayari umeingia nchini tangu Machi 16, mwaka huu, kwa mgonjwa wa kwanza Isabella Mwampamba (46) kupatikana mkoani Arusha.

Pia idadi iliongezeka Machi 18 mwaka huu hadi kufikia wagonjwa watatu, baada ya wagonjwa wengine wawili kutoka Zanzibar na mwingine jijini Dar es Salaam ambao walitangazwa kuwa na COVID-19 na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

# Kanisa Anglikana latenga siku ya maombi maalum

**Na Romana Mallya**

KANISA la Anglikana Tanzania limezitaka dayosisi zake zitenge siku maalum ya maombi kwa ajili ya kuliombea taifa dhidi ya janga la virusi vya corona ambavyo tayari Watanzania watano wameambukizwa.

Kwa mujibu wa taarifa ya kanisa hilo kwa dayosisi zote, Siku ya Ijumaa Kuu itakuwa ya ibada ya pamoja ya Anglikana Tanzania kuombea taifa dhidi ya ugonjwa huo.

Tamko hilo limetolewa jijini Arusha jana katika kikao cha Nyumba ya Maaskofu cha mwaka wa Bwana Yesu 2020.

“Tunayo imani kubwa kwamba hakuna lisilowezekana kwa Mungu. Ugonjwa huu umetangazwa katika kipindi cha Kwaresma ambapo tupo katika majira ya toba na kufunga kuelekea Pasaka.

“Tunahitaji kuendelea kupiga magoti na kujinyenyekeza mbele za Mungu kwa maombi ya kuutafuta uso wa Mungu huku tukiacha njia zetu mbaya,” ilisema taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema kanisa hilo linawaombea waathirika wote kwa kusimama kwenye maombi na watu wote kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuzingatia maelezo ya serikali yenye lengo la kujikinga na kuwakinga wengine dhidi ya ugonjwa huo.

Pia ilisema pale inapolazimu kukutana wahimizane kujitenga kwa umbali uliostahili.

“Tujitahidi kutoa taarifa kwenye mamlaka husika mara kwa mara tunapobaini kuwapo kwa dalili za maambukizi ya ugonjwa kama serikali inavyohimiza,” ilisema.

Kanisa hilo pia limehimiza milango na madirisha ya kanisa kuachwa wazi wakati wa huduma na ibada ili kuwezesha hewa kuingia.

“Kuhusu wagonjwa, tunahimiza wahudumiwe kwa maombi ya mbali kwa kuzingatia njia zinazohusu mikusanyiko ili kuepuka maambukizi zaidi,” alisema.




# Mwalimu anusurika kuuawa na wananchi

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MWALIMU wa Shule ya Msingi Mitonji katika Kijiji cha Mitonji Kata ya Mbuyuni katika Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, John Mandanda amenusurika kuuawa na wananchi wenye hasira kali, baada ya kuwacharaza viboko wanafunzi hadi mmoja kupoteza fahamu.

Mwanafunzi huyo wa darasa la sita (jina linahifadhiwa) anadaiwa kupoteza fahamu kwa zaidi ya saa moja.

Kutokana na tishio la kuchapwa na wananchi hao walimu walimwokoa mwenzao kwa kumfungia ndani ya ofisi, huku wananchi hao waliotaka kumpa kichapo wakiwa wamebeba marungu, mashoka na silaa zingine za jadi.

Akizungumza na Nipashe jana kwa njia ya simu, Ofisa Elimu Msingi Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, Elizabeth Mlaponi, alisema mwalimu huyo alifanya tukio hilo juzi majira ya saa 5:00 asubuhi wakati wanafunzi walipokuwa wakiingia darasani baada ya mapumziko mafupi.

Alisema mwalimu huyo akiwa shuleni hapo siku ya tukio, alitoa adhabu kwa baadhi ya wanafunzi ambao inaelezwa kuwa walikuwa wamechelewa kuingia darasani baada ya kengere ya kuingia darasani kupigwa, huku wakiwa nje ya darasa.

Mlaponi alisema mwalimu huyo baada ya kuona wanafunzi hao wamechelewa kuingia darasani, aliamua kuwacharaza viboko wanafunzi hao kila mmoja viboko viwili. Alisema baada ya kutoa adhabu ndipo mmoja wa wanafunzi hao baada ya kuchapwa kiboko kimoja alianguka chini ya sakafu na na kumsababishia majeraha kwenye baji la uso wake.

"Tulipopata taarifa juu ya tukio hili la mwalimu kumchapa mwanafunzi na kumsababishia majeraha, tulifika hadi shuleni hapo na tulikuta wananchi wamezingira eneo la ofisi ya mwalimu mkuu ambapo alikuwa amefungiwa ndani na walimu wenzake wakimataka mwalimu huyu atolewe nje ili wampige,"alisema Mlaponi

Afisa elimu huyo alieleza kuwa suala la mwalimu huyo wanaendelea kulishughulikia ikiwa ni pamoja na kulepeka katika ngazi za juu ikiwamo ofisi ya mkuu wa wilaya kwa ajili ya utekelezaji zaidi. Mwenyekiti wa serikali ya kijiji cha Mitonji, Shabani Nguseka, alisema ofisi ya serikali ya kijiji na baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mitonji walipata taarifa hizo kutoka kwa baadhi ya wanafunzi wenzake wa shule hiyo wakieleza kuwa mwenzao amepigwa hadi kuzimia.

Mguseka alisema baada ya wananchi kupata taarifa hizo waliandamana hadi shuleni hapo na wakishinikiza kutaka mwalimu huyo wampe kichapo kama alivyomchapa mwanafunzi. Alisema uongozi wa serikali ya kijiji ulishirikiana na familia ya mwanafunzi huyo kwa kumchukua mwanafunzi kumpeleka kwenye Zahanati ya kijiji cha Nagaga kwa ajili ya kupata matibabu ya awali.

**BEST GROUP (T) LIMITED**
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

Kwa idhini tuliyopewa na **Banc ABC,** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana za wadaiwa wao, ambazo ni Nyumbailivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea.

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | SARA NICAS YABU | Kiwanja na.102, Kitalu "H"Chenye hati na.91257,Kilichopo eneo la Kitopeni ,Bagamoyo<br>Kiwanja na.104,Kitalu"H"Chenye hati na.91260,kilichopo eneo la Kitopeni Bagamoyo | 11/04/2020 |
| 2. | MJULE CIARATA NDEGE | Nyumba ya makazi yenye kiwanja na.991/253,Kitalu "C"Hati na.96607,Iliyopo maeneo ya Mtoni Kijichi - Manispaa ya Temeke | 18/04/2020 |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa Au kuchukua mshindi wa pili.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE: +255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Banc ABC
Bib titi Mohamed Road,
P.O.BOX 31
DAR ES SALAAM
Tel:+255 222119422



Janeth Magufuli (kulia), akikabidhi vitu mbalimbali kwa wawakilishi wa walezi na watoto wanaolelewa katika Kituo cha Nyumba ya Matumaini, katika hafla ya utoaji misaada kwa vituo vya kulelea watoto wenye mahitaji, iliyofanyika Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Membe akoleza moto tume huru uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Bernard Membe, amesema tume huru ya uchaguzi haikwepeki ili kuwa na uchaguzi huru na haki.

Kwa mujibu wa taarifa aliyoandika kwenye ukurasa wake wa Twitter, alisema jambo hilo alilizungumza hata alipoitwa na kamati ya maadili ya kilichokuwa chama chake kwa ajili ya kuhojiwa Februari, mwaka huu.

"Nilisema hili kwenye kamati ya maadili na ninasema tena. Kwa mazingira ya kisiasa yaliyopo tunahitaji tume ya uchaguzi ambayo ni huru, yenye uwakilishi na uwazi kwa ngazi ya taifa na wilaya. Ninaunga mkono kwa nguvu zote sauti zote za kudai hili," alisema.

Februari 28, mwaka huu, Kamati Kuu ya CCM ilitangaza kumfukuza Membe ambaye amewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa katika serikali ya awamu ya nne na Mbunge wa Mtama kwa miaka 15, kwa kile kilicholeezwa ni kwenda kinyume cha matakwa ya chama hicho.

Wakati Membe akivuliwa uanachama, Katibu Mkuu wa zamani wa chama hicho, Abdulrahman Kinana, alipewa karipio na kutakiwa kutogombea nafasi yoyote ndani ya chama hicho kwa miezi 18, huku Katibu Mkuu mwingine mstaafu, Yusuph Makamba, akiomba msamaha na hatimaye kusamehewa.

Kwa muda mrefu vyama vya upinzani vimeendelea kudai tume huru ya uchaguzi kwa madai kuwa iliyopo sasa haiwatendei haki kutokana na muundo wake.

Hivi karibuni, Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, alisema chama hicho kitaanza mikutano ya hadhara ya kudai tume huru ya uchaguzi kwa kuwa iliyopo kimuundo haiwatendei haki kwa kuwa watendaji wake ni wateuliwa wa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa CCM.

Februari mwaka huu, Mbowe akiwa kwenye mziba wa Elias Mwingira, baba wa kiongozi wa kanisa la Efatha, Mtume na Nabii Josephat Mwingira, alisema ni lazima kuwa na tume huru kabla ya uchaguzi wa Oktoba, mwaka huu.

Pia Januari 29, mwaka huu, alisema amemwandikia Rais akiomba serikali kufanya mabadiliko ya sheria yatakayowezesha kuunda kwa tume huru kabla ya Oktoba.

Naye Kiongozi Mkuu wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, alikaririwa mara kadhaa akisema kuwa tatizo si uchaguzi kufanyika bali ni tume huru ambayo itatenda haki kwa kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na haki.

Zitto akizungumza kwenye mkutano mkuu wa chama hicho, alisema msimamo wa chama hicho katika chaguzi zijazo ni kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi, ili uchaguzi wa Oktoba usiwe na dosari kama zilizojitokeza kwenye uchaguzi uliopita.

Kiongozi huyo alikwenda mbali zaidi na kuvitaka vyama vyote kuungana kudai tume hiyo.

Naye Mwenyekiti wa Cuf, Prof. Ibrahim Lipumba, alisema chama hicho kinahitaji katiba mpya ili uchaguzi uwe huru na haki lazima kuwe na tume huru. Machi mwaka huu, Mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi, James Mbatia, alisema tangu kuasisiwa kwa chama hicho mwaka 1991 hitaji limekuwa katiba mpya ambayo ndani yake itakuwa na tume huru ya uchaguzi.

Hata hivyo, Machi 6, mwaka huu, Katibu Mkuu wa CCM, Bashiru Ally, alipotembea vyombo vya habari vya IPP, alisema tume hiyo iko huru na kwamba uchaguzi utakuwa huru, haki na salama.

"Nawahakikishia Serikali za CCM zina dhamana ya kuhakikisha uchaguzi unafanyika katika mazingira huru, haki na salama," alisema.

"Rais Magufuli amekusanya kodi, nawahakikishia tume itapata fedha za kutosha...kwa mara ya kwanza tutaendesha uchaguzi bila kutumia fedha za wafadhili, hiyo nayo ni uhuru, tume tegemezi haiwezi ikaendesha uchaguzi huru, unaweza kuona huru kwa macho lakini kuna mtu kaleta fedha, anakuleta tekonolojia ikiziba unaletewa mtaalamu kuzibua," alisema.

"Wakati wanafanya vizibo yeye ndiyo anajua kizibo gani kimewekwa na akichelewa mnatafutana manakaa siku saba hamjapata matokeo...uhuru wa uchaguzi ni pamoja na nchi kugharamia uchaguzi wake wenyewe na kutumia wananchi wake kusimamia uchaguzi," alisisitiza.

"Mahitaji ya tume huru ni zaidi ya tume yenyewe, mahitaji ya uchaguzi huru na haki ni zaidi ya kazi zitakazofanywa na tume, tunanze kujiandaa kujenga imani katika tume, polisi, vyama vya siasa na wapiga kura,"alisema.

Januari mwaka huu, Rais John Magufuli alipokutana na mabalozi wa nchi zenye balozi nchini, aliwahakikishia kuwa uchaguzi wa mwaka huu utakuwa huru, amani na haki.

Pia Ubalozi wa Marekani nchini, ulitoa taarifa ukitaka kuharakishwa kwa uanzishwaji wa tume huru ya uchaguzi na kuteuliwa mapema kwa waangalizi wa uchaguzi wa kitaifa na kimataifa wanaoaminika watakaofuatilia uchaguzi kwa kipindi kirefu na kifupi.

## Mawaziri wapitisha bajeti dola mil. 94/- SADC

Na Gwamaka Alipipi

BARAZA la Mawaziri la nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) limepitisha bajeti ya dola za Marekani milioni 94.319 (zaidi ya Sh. bilioni 200) kwa mwaka wa fedha ujao.

Katika bajeti hiyo, vipaumbele vikuu vinne vimeainishwa ambavyo ni uendelezaji wa viwanda, ujenzi wa miundombinu kama vile barabara, kushughulikia uhimilivu wa kisiasa, ulinzi na usalama na kuboresha afya, elimu, jinsia na mazingira.

Katibu Mtendaji wa SADC, Dk. Stergomena Tax, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa kufunga mkutano wa Baraza la Mawaziri wa SADC lililojumuisha mawaziri wa fedha na mipango, viwanda na biashara, mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa.

"Mwaka mpya wa fedha wa SADC 2020/21 unaanza Aprili na mwaka wa fedha 2019/20 unamalizika Machi. Leo (jana) mojawapo ya agenda iliyokuwa inajadiliwa na Baraza la Mawaziri ni upitishwaji wa bajeti ya mwaka mpya wa fedha, hivyo dola za Marekani milioni 94,319,815 zimepitishwa," alisema.

Dk. Tax alisema Agosti Mosi, mwaka huu, SADC itasherehekea miaka 40 tangu ilipoanzishwa na maadhimisho hayo yatafanyika Msumbiji wakati wa mkutano wa wakuu wa SADC.

Kuhusu mkutano huo kufanyika kwa njia ya video, Dk. Tax alisema ulikuwa na mafanikio makubwa na kwamba nchi 13 zilishiriki kikamilifu.

Alisema fedha zilizotumika kununua mtambo wa mawasiliano zilitolewa na sekretarieti ya SADC, lakini walipata mdau wa kuunganisha mawasiliano kutoka Shirika la Mawasiliano la Tanzania (TTCL).

Kuhusu ugonjwa virusi vya corona, Dk. Tax alisema katika ukanda wa SADC umeshasambaa kwenye nchi mbalimbali, hivyo wamekubaliana kuwa na mkakati wa pamoja na kila nchi itasimamia mkakati huo.



Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), wakiondoka chuoni hapo, jijini Dar es Salaam jana, kufuatia agizo la serikali la kufunga vyuo vyote nchini kwa muda wa siku 30 kutokana na tishio la ugonjwa wa corona. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mdee, Bulaya watoka hospitalini

Na Mary Geofrey

VIONGOZI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Mbunge wa Kawe Halima Mdee na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, waliokuwa wamelazwa hospitalini wakipatiwa matibabu kutokana na majeraha ya kupigwa, wameruhusiwa baada ya hali zao kuendelea vizuri.

Viongozi hao wanadaiwa kupigwa na kuvunjwa mikono na miguu na maofisa wa Magereza Ijumaa, wiki iliyopita walipokwenda Magereza ya Ukonga kumpokea Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe.

Viongozi hao pamoja na Meya wa Ubungo, Boniface Jacob, Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya, pamoja na wanachama 27 wa chama hicho, wanatuhumiwa kuvamia Gereza la Segerea na kufanya fujo, kuwavamia maofisa wa Magereza na kuwazuia kufanya kazi zao.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Chadema, Tumaini Makene, aliiambia Nipashe jana kuwa, viongozi hao wanaendelea vizuri na waliruhusiwa Jumanne.

"Hali zao zinaendelea vizuri na wamesharuhusiwa kutoka hospitali kwa sasa wapo nyumbani," alisema Makene.

Akizungumza na waandishi wa habari Jumapili wiki iliyopita, Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema: "Upelelezi wa kesi umekamilika na kesho (Jumatatu iliyopita) jalada litapelekwa kwa Mwanasheria wa Serikali alipitie kwa namna itakavyomfaa atapeleka mahakamani wakajibu tuhuma hizo."

Alisema askari Magereza walimpigia simu wakiwaeleza kuwa, kuna watu wanataka kuvamia eneo la Magereza na wanafanya fujo, hivyo waliondoka kwenda eneo la tukio kwa kuwapeleka askari wa kanda pamoja na askari wa kutuliza ghasia.

Jumanne iliyopita, Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, iliwahukumu vigogo saba wa Chadema akiwamo Mbowe na mwanachama mpya wa CCM, Dk. Vincent Mashinji, kulipa faini ya Sh. milioni 350.

Vigogo hao walilipiwa faini kupitia michango ya wananchi mbalimbali na kuachiwa huru.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**President's Office – State House**
**TANZANIA SOCIAL ACTION FUND**

**EXTENSION OF DEADLINE FOR SUBMISSION OF TENDERS**

The Tanzania Social Action Fund on 4th March, 2020 invited the following Tenders from eligible suppliers and service providers:
i. Tender No. TZ-TASAF-148779-GO-RFB to Supply ICT Consumables
ii. Tender No. TZ-TASAF-148787-GO-RFB to Supply Stationery
iii. Tender No. TZ-TASAF-148782-GO-RFB to Supply Motor Vehicle Spare Parts
iv. Tender No. TZ-TASAF-161184-NC-RFB for Printing Handbooks, Manuals, Publicity Materials and Reports

The deadline date for submission and public opening set and announced in the advert was 31st March, 2020.

The Tanzania Government has issued some directives to control spread of the coronavirus (COVID19) epidemic following presence cases in the country.

One of the directives issued by the Government is to ban public gatherings including meetings.

From this scenario, we would like to inform prospective bidders and the general public that the deadline date for submission and subsequent public tender opening meeting is changed from 31st March, 2020 to 4thMay, 2020 if the quarantine is ended by that date otherwise a forward date will be announced before 4thMay, 2020

**The Executive Director,**
**Tanzania Social Action Fund,**
**4th Floor, PSSSF Plaza, JakayaMrishoKikwete Road,**
**P. O. Box 2719,**
**Dodoma, Tanzania**

215673802

**UNHCR**
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

**INVITATION TO BID (ITB)**
**ESTABLISHMENT OF LOCAL FRAME AGREEMENTS FOR SUPPLY AND DELIVERY OF ASSORTED NON-FOOD ITEMS**

**1. Background:**

The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites reputable and qualified suppliers and manufacturers to submit firm offers for Establishment of multiple Frame Agreements for the supply and delivery of any or all of the below listed Non-Food Items.

**2. Requirement:**

| TENDER REFERENCE NUMBER | TENDER ITEM DESCRIPTION |
|---|---|
| ITB/2020/SUP/006 | Plastic Jerry Cans |
| ITB/2020/SUP/008 | Sanitary Napkins (Re-Usable Pads) |
| ITB/2020/SUP/009 | Sleeping Mats |
| ITB/2020/SUP/010 | Kitchen Sets |
| ITB/2020/SUP/011 | Solar Lamps |
| ITB/2020/SUP/012 | Mosquito Nets |

**3. Eligibility:**

Manufacturers, authorized resellers, wholesalers, or traders duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's needs are invited to participate in the bidding process.

The tender documents can be collected from the following UNHCR Offices:

UNHCR Representation Office Tanzania
Plot 1658 Masaki, Rufiji Street
P.O Box 2666 - **Dar es Salaam**

UNHCR Sub- Office Kibondo
Kabigwa (Near TANESCO)
P.O. Box 49, **Kibondo**

UNHCR Field Office Kasulu
Kimobwa (Mlimani Area)
P.O. Box 332 - **Kasulu, Kigoma**

UNHCR Field Unit Mwanza
Mwanza Airport
P.O. Box 2273 – **Mwanza**

215664402

**CRUCIAL DATES FOR THIS REQUEST FOR PROPOSAL**

| | |
|---|---|
| Deadline for receiving requests for clarification | Monday 23rd March 2020 at 16.00 hours EAT |
| Deadline for submission of offers | Wednesday 08th April 2020 16.00 hours EAT |

*UNHCR tenders are free of charge, no fees are charged to collect the tenders.*

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Funzo la corona kwa sekta ya afya

**POLENI** Watanzania kwa hofu ya homa ya corona ambayo inamfanya kila mmoja kuwa na woga kutokana na ugonjwa huo unaoua kwa muda mfupi.

Uwapo wa corona umekuja wakati ambao kila mmoja anatakiwa kuwajibika, lakini zaidi sekta ya afya ambayo ina wajibu mkubwa wa kipekee kusimamia na kuhakikisha ulinzi na usalama wa afya kwa wananchi wote.

Tunasema haya kwa sababu ina jukumu kubwa la kuboresha mifumo ya afya na kuweka mikakati ya kudhibiti maambukizi na kutibu wagonjwa.

Tunaona kuwa huu ni wakati pia wa kuhakikisha kuwa kuna fedha za kutosha za kudhibiti tatizo hilo la kuwafikia watu wote bila kujali wanaishi mjini au kijijini.

Kuwapo kwa maradhi haya kunahitaji na kuulazimisha uongozi wa kitaifa kuwa na ridhaa ya kisiasa ya kutumia rasilimali kuanzia fedha, wataalamu na muda na vifaa kutibu na kuokoa maisha ya watu wasidhuriwe na corona.

Tunafurahishwa na hatua na nia ya serikali ya kudhibiti ugonjwa huu kwa kufunga vyuo vikuu na vya kati, shule na kupiga marufuku mikusanyiko mikubwa isiyo na sababu na pia kuboresha mifumo ya afya na kujitahidi kukabiliana kwa nguvu zote na maradhi haya.

Kwa ujumla, tunaona kuwa funzo linalotokana na corona ni la kipekee na hasa kuona umuhimu wa kuboresha miundombinu ya afya ikiwamo kujizatiti kuwa na huduma na wataalamu wa kutosha ndani ya hospitali zetu kuliko kutegemea na kuamini kuwa matibabu bora yanapatikana nje ya nchi.

Funzo linalotokana na corona ni kwamba haiwezekani kuwapeleka wagonjwa wa maradhi hayo nje ya nchi kwa matibabu. Kama vile kuwapeleka Afrika Kusini, Ulaya au India.

Kwa hiyo, kama ambavyo Tanzania imefanya bidii kuimarisha sehemu kubwa ya sekta ya afya kwa kuanzisha vitengo vya matibabu ya moyo, saratani, mifupa na mishipa ya fahamu pamoja na figo, ndivyo sasa taifa linapaswa kujivunia na kutembea kifua mbele kuwa kila jambo linawezekana iwapo tutatia nia.

Halikadhalika pamoja na juhudi hizo tunapenda kuishauri serikali kufikiria uwezekano wa kuanzisha kitengo maalumu cha magonjwa ya dharura.

Tunashauri haya kwa sababu ukanda wa Afrika umekuwa na magonjwa ya dharura na hatari kama ulivyokuwa mlipuko wa homa ya ebola, dengue, chikungunya na sasa corona.

Tunaamini kuwa kwa kuwa na kituo kama hicho kuna uwezekano wa kudhibiti kwa urahisi lakini pia kuwa na uwezo wa kupunguza ukubwa wa tatizo kwa kuwa kituo kitakuwa na fedha za kutosha, wataalamu kuanzia wauguzi, madaktari, wataalamu wa maabara zikiwamo zinazohamishika (mobile laboratories), vifaa kama magari, helkopta, droni na vifaa tiba ikiwamo hadubini za kisasa zaidi.

Tunaona kuwa kuwapo kwa kituo na wataalamu hao kutasaidia kupunguza ugumu wa tatizo na kufanikisha wepesi katika kukabiliana nalo.

Pamoja na mambo mengine ni wazi kuwa miaka ya nyuma ni kama sekta ya afya ilikuwa zaidi ikihudumiwa na wahisani, lakini tunaipongeza serikali leo kwa kuisimamia kikamilifu sekta hii na kuiboresha kwa kutumia fedha za ndani.


Jitihada hizo zimefanikisha kutafuta na kuongeza fedha kwa ajili ya sekta hiyo, kufunza wataalamu wa kada mbalimbali, kuboresha huduma katika hospitali za wilaya, rufani na hospitali maalumu za kikanda na kudhibiti ukusanyaji holela wa mapato kwenye huduma za afya ikiwamo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.


Tutaendelea kuungana na serikali kupambana na corona kwa kuielimisha jamii kuhusu kujikinga na kudhibiti ugonjwa huu.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

Na Yasmine Protace

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wakopaji makundi maalumu warejesha mikopo yao

**KILA** wakati inajulikana kwamba, mkopo ndio mkombozi wa kila kitu katika sura ya maendeleo ya kijamii na kuchumi. Mtu anachukua na kisha akajipanga namna ya kuikabili.

Siku zote mikopo imekuwa mkombozi kwa watu mbalimbali au taasisi, kutokana na kutumika katika kujiongezea mapato ndani ya maeneo husika.

Mikopo inatolewa katika makundi mbalimbali, ili mtu katika nafasi ya mmoja mmoja au taasisi, lengo ni kuyawezesha maeneo hayo kuinuka kiuchumi.

Tumeziona taasisi mbalimbali ambazo zinazotoa, mikopo kwa makundi mbalimbali, ikiwamo kampuni za simu ambazo nazo zinatoa mikopo.

Pamoja na kutoa mikopo na kampeni za simu, kila anayechukua mkopo, lazima alipe na tiba kulingana na viwango vilivyoidhinishwa.

Mikopo hiyo inakusanywa na pale inapotolewa na riba, inakusanywa na taasisi hizo, kisha unafanyika mzunguko ili kuwawezesha na kupata mikopo.

Katika baadhi ya taasisi, unapochukuliwa mkopo una masharti kwamba mtu anapochelewa kurejesha, hapatawi fursa nyingine kulipa.

Imeshatokea, katika mikopo hiyo, kuna kampuni au taasasi zimekuwa zikiuza mali za wateja wasiolipa mikopo.

Tukirejea kwa kina, mikopo ambayo Rais John Pombe Magufuli, aliagiza itolewe kwa wanawake, walemavu na vijana, aliweka wazi kwamba itolewe bila ya kuwatoza riba.

Pamoja na fadhila hiyo ya kiserikali, bado kuna baadhi ya vikundi vilivyochukua mikopo na kushindwa kurejesha kwa wakati,

> **Pamoja na fadhila hiyo ya kiserikali, bado kuna baadhi ya vikundi vilivyochukua mikopo na kushindwa kurejesha kwa wakati, hali inayokwamisha wengine hata wakakosa fursa za kupata mikopo hiyo.**

hali inayokwamisha wengine hata wakakosa fursa za kupata mikopo hiyo.

Baadhi ya watu wamekuwa wakilalamikia, kwamba wanakosa mikopo. Hivi karibuni, Diwani wa Kata ya Mabibo, jijini Dar es Salaam, Kassim Lema, anasema kuwa Wilaya ya Ubungo, imetoa mikopo zaidi ya shilingi bilioni tatu, kuviwezeshwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu.

Anasema mbali na hilo, mpaka sasa kuna kiasi cha Sh. milioni 700 pekee ndio zimerudishwa na alinukuliwa akitamka hivi:

"Tumetoa zaidi ya Sh. bilioni tatu, kuvipatia vikundi vya wanawake, walemavu na vijana, lakini mpaka sasa marejesho yaliyopokelewa ni Sh. milioni 700."

Lema anasema, wale wasioelewa wataona kama mikopo haijawahi kutolewa, lakini waelewe kuwa mikopo imeshaanza kutolewa, lakini baadhi ya wanavikundi sio waaminifu.


Anafafanua kwamba, mikopo kutorejeshwa kwa wakati katika Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo, kamati husika imekaa na kutafakari jinsi ya kuanza kuwachukulia hatua wanavikundi ambao hawajarejesha mikopo husika.

Diwani Lema anafafanua kiasi cha shilingi bilioni tatu kilichogawiwa katika makundi hayo, kwamba kinamama walipata shilingi bilioni 1.6, vijana walipata shilingi bilioni 1.5 na walemavu Sh. milioni 180.

Anasema, pamoja na mikopo kutolewa bila ya riba, lakini baadhi ya vikundi vimeshindwa kuirejesha mikopo kwa wakati.

MJADALA

# Foleni za magari Dar zahitaji usimamizi zaidi




**Na Sabato Kasika**

DAR ES SALAAM ni kati ya miji inayokabiliwa na foleni za magari kila kuchao na kusababisha wakazi wake kuchelewa kwenye shughuli zao, zikiwamo za uzalishaji mali.

Kwa sasa imekuwa kawaida, kuona safari ambayo mtu anaweza kutumia kwa dakika kadhaa, inamchukua muda mrefu zaidi, hapana kushangaa hata saa kadhaa ndio anafika anakoenda.

Hali hiyo imekuwa ikitajwa kuchangia upotevu wa fedha, kutokana na kwamba watu hawafiki kwenye kazi kwa wakati, hata uzalishaji mali kupungua na kusababisha hasara.

Waapo baadhi ya watu wanaonufaika na foleni hizo na hasa wafanyabiashara, wapo wadogo wanaotembeza bidhaa zao kwenye foleni za magari.

Foleni za magari Dar es Salaam, zina hasara kwa upande mmoja na faida upande mwingine wa shilingi. Pamoja na hayo, ni tatizo linalotakiwa kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Ninasema hivyo, kwa sababu upande wa hasara ni kubwa kuliko faida, Wapo watu wachache wanaouza biashara ndogo kwa ajili ya maisha yao ya kila siku, lakini kwa uchumi wa nchi kuna hasara kubwa.

Hiyo inatokana na ukweli muda wa kuzalisha mali viwandani na kwingineko unapotelea barabarani, wakati magari ya abiria ambayo kimsingi yanatakiwa kuwahisha wafanyakazi sehemu za uzalishaji mali, huwa kwenye foleni,

Umefika wakati sasa wa kutafuta mbadala wa njia za kumudu foleni hizo, wakati barabara za juu zikiendelea kujengwa kwenye maungio ya baadhi ya maeneo, ikiwa namna ya kufafuta ufumbuzi wa kudumu.

Foleni za magari za Dar es Salaam, baadhi huenda zipo za lazima, lakini kuna nyingine wadau wa mawasiliano wakisimamia vizuri, zinaweza kuisha na kusaidia watu kuwahi.

Kwa mfano, kuna foleni za kizembe zinazozsababishwa na baadhi ya madereva wa daladala, ambao badala ya kusimama kwenye vituo na kushusha au kupakia abiria, wanasimama katikati ya barabara.

Wapo wanaosimama vituoni, wakiegesha magari kwa mtindo wa kuwazuia wenzao wasipite, hali inayo sababisha foleni zisizo za lazima na kuchelewesha wengine.

Baadhi ya askari wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, nao wanalalamikiwa kusababisha foleni, wanapokuwa kwenye makutano ya barabara.

Ingependeza zaidi, askari wangeangalia madereva wanaovunja sheria za usalama barabara na kuwakamata, ikiwa mbinu mojwapo ya kupata ufanisi.

Wakifanya hivyo watakuwa wamesaidia wakazi wa Dar es Salaam kutopoteza muda bure, kwa sababu ambazo wakati mwingine ziko ndani ya uwezo wa madereva wa daladala na hata askari hao.

Foleni zimekuwa zikisababisha baadhi ya watu kulalamika na hata kulazimika kukodi bodaboda au bajaji, ili wawahi kwenye shughuli zao, hali iliyo sawa na kuwaharibia bajeti.

Ni kweli barabara za juu zimejengwa, mfano katika eneo la Tazara na inaendelea kujengwa Ubungo, lakini hazitakuwa na manufaa iwapo foleni zisizo za lazima hazitadhibitiwa.

Badala yake zitabaki kuwafaidisha wafanyabiashara wadogo ambao wamekuwa wakifurahia foleni kunadi biashara zao za mkononi.

Ikumbukwe kuwa, mbali na ujenzi wa barabara za juu, tayari kuna barabara za mchepuko kwenye baadhi ya maeneo, lakini bado hazitoshi kutokana na wingi wa magari, ila la muhimu kuangalia upya mambo mawili.

Mambo hayo ni uegeshaji wa magari kwenye vituo, unaofanywa na madereva wa daladala, ambao una mchango mkubwa kwenye foleni za magri, pia uondoaji wa askari kwenye maeneo ambayo kuna taa.

Kwa wanaotumia usafiri wa umma, watakuwa wamewahi kusikia malalamiko ya abiria kuhusu uegeshaji mbovu wa magari unaofanywa na madereva wa daladala pia uongozi wa magari unaofanywa na trafiki.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed




ewura
Energy and Water Utilities Regulatory Authority
ISO 9001:2015 Certified

TAARIFA KWA UMMA

*19 Machi,2020*

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inawatangazia wadau wake wote na umma kwa ujumla kuwa, pale **pasipo na ulazima wa kufika katika Ofisi za EWURA,** watumie mawasiliano ya simu na mtandao kupata huduma.

Hatua hii inachukuliwa ili kuendelea kukabiliana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).

Wadau wanashauriwa kutumia mawasiliano yafuatayo:-

Simu: (1) 0800110030 (BURE)
(2) +255-26 2329002-3

Barua pepe: info@ewura.go.tz

**Imetolewa na:**
**MKURUGENZI MKUU**

215674402

# MSD kusambaza maski, sabuni kudhibiti corona

**Na Elizabeth Zaya**

BOHARI ya Dawa (MSD), imesema endapo wafanyabiashara wa bidhaa zinazosaidia kujikinga na maambukizo ya virusi vya corona wataendelea na tabia ya kupandisha bei ya bidhaa hizo, itabidi iingize yenyewe vifaa hivyo mtaani.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Laurean Mwanakunu, alipozungumza kwenye mahojiano na Kituo cha ITV.

Alisema MSD haifanyi kazi ya kuuuza dawa au bidhaa zinazotumika kwenye masuala ya afya, lakini itabidi ifanye kazi hiyo ya kuvisambaza mitaani ili kuwadhibiti wafanyabiashara wenye nia mbaya, wanaotumia tishio la ugonjwa wa corona kuwaumiza wananchi.

"Kawaida MSD hatufanyi kazi ya kuwauzia watu binafsi dawa au mmoja mmoja, sisi tunadili na vituo vinavyotoa huduma za afya pekee, lakini nawaambia wafanyabiashara kwamba wakiendelea hivi, soko nitalijaza vifaa vya MSD ili vitu vyao wanavyowaibia wananchi viwadodee," alisema.

"Tungependa wote tufanye kwa pamoja, sisi tuendelee kuhudumia vituo vya afya na wao waendelee kuhudumia wananchi. Hatusemi kwamba wauze kama bei ya serikali, lakini hawapaswi kupandishia bei kama wanavyofanya sasa," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu suala hilo, Mwanakunu alitolea mfano vitakasa mikono ambavyo bei yake halali ni Sh. 2,500 lakini kwa sasa wafanyabiashara wamepandisha zaidi bei kwa kuviuza kwa Sh. 5,000.

Alisema vitakasa mikono hivyo vya lita tano bei yake halali ni Sh. 85,000, lakini wafanyabiashara kwa sasa wanauza hadi Sh. 200,000. Aliongeza kuwa vidonge vinavyotumika kwa kuwekwa kwenye maji ya kunawa mikono, bei yake halali kwa kidonge kutoka MSD ni Sh. 360, lakini wafanyabiashara wanauza Sh. 5,000. Alisema kopo lote la vidonge hivyo ambavyo viko 100, kawaida huuzwa Sh. 36,000 lakini wafanyabiashara kwa sasa wanauza Sh. 500,000.



Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, na kuwataka Watanzania kuwa makini dhidi ya tishio la ugonjwa wa corona. Kulia ni Mkurugenzi wa Haki za Binadamu na Sheria wa chama hicho, Salvatory Magafu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wanafunzi wahaha kupata usafiri

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

CHANGAMOTO kubwa ya usafiri imeibuka katika kituo kikuu cha mabasi cha Msamvu baada ya wanafunzi wa maeneo mbalimbali kufunga shule kwa wakati mmoja, huku hofu kubwa ya abiria ikiwa ni hatari ya maambukizo ya virusi vya corona.

Mwandishi wa habari hizi aliyefika kwenye stendi hiyo, alikuta idadi kubwa ya wanafunzi, wakiwa wamesimama kwa makundi wakisubiri usafiri, huku mabasi yakipita yakiwa yamejaa na yanayoanzia safari Morogoro yakipatikana machache kwa kugombewa.

Baadhi ya wanafunzi hao, Apolina David, Princess Alvin na Festo Mapunda, wakakiri hali ni mbaya kituoni hapo kutokana na msongamano mkubwa uliopo.

"Angalau wakati mwingine huwa tunafunga shule kwa awamu, tunapishana na magari mengine yanatufuata shuleni, lakini hii dharura imefanya wote tujazane stendi, na hatuna uhakika wa kusafiri," alisema Festo.

Wanafunzi hao walishauri kwa dharura kama hiyo ni vyema serikali ingetoa usafiri wa bure wa magari ili kuondoa msongamano unaoweza kutishia afya ya wakazi hasa wakati huu wa mlipuko wa magonjwa.

Katibu wa Umoja wa Wasafirishaji kituo cha Mabasi Msamvu, Hamza Rashid, aliwashauri LATRA, kurahisisha upatikanaji wa vibali vya usafirishaji ili kuondoa hatari ya maambukizo.

## Mitihani ya kidato cha sita, ualimu yasitishwa

**Na Beatrice Moses**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesitisha Mitihani wa Taifa wa Kidato cha Sita na wa ualimu iliyokuwa ifanyike Mei mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Baraza la Mitihani la Taifa (Necta) lilitangaza uamuzi huo juzi baada ya serikali kutangaza kufunga shule na vyuo vyote kwa kipindi cha mwezi mmoja kuanzia Machi 17 mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Avemaria Semakafu, akizungumzia uamuzi huo jana, alisema huenda pia ukawaathiri wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha tano mwaka huu, ratiba ya masomo ikionyesha wanatakiwa kuripoti shuleni Julai mwaka huu.

"Serikali imetangaza kuzifunga shule na vyuo kwa mwezi mmoja ili kuangalia hali itakavyokuwa, hivyo ni wazi ratiba ya mtihani nayo itabadilika, sasa ni kuomba Mungu kusitokee tena maambukizo mapya," alisema. Kiongozi huyo wa wizara alisema ni ngumu kuzungumzia ratiba za kuanza kwa masomo ya kidato cha tano kwa kuwa bado hali haijajulikana itakavyokuwa.

Necta ilitangaza juzi kuahirisha mitihani hiyo iliyokuwa imepangwa kuanza Mei 4 mwaka huu hadi pale itakapotoa taarifa nyingine.

Baraza hilo pia liliwataka maofisa elimu wilaya kuwapa taarifa wakuu wa shule na vyuo vya ualimu nchini ili wawajulishe watahiniwa kuhusu kuahirishwa kwa mitihani hiyo.

Machi 17 mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kufungwa kwa shule zote za awali, msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na baadaye vyuo vya kati na vyuo vikuu ili kudhibiti misongamano inayoweza kuchochea kusambaa kwa virusi vya corona.

Majaliwa aliagiza wahusika kufanya utaratibu kwa ajili ya wanafunzi waliotakiwa kufanya mitihani ya kidato cha sita na ualimu.

Uamuzi huo wa serikali ulichukuliwa ikiwa ni siku moja baada ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia. Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, kuthibitisha kuwapo kwa mgonjwa wa corona nchini.

HABARI KITAIFA

# Waziri atoa maagizo tishio ujangili

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amekiagiza Kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU) Kanda ya Kaskazini kuongeza mbinu katika kukabiliana na ujangili wa wanyamapori wadogo wanaouawa kwa ajili ya kitoweo na baadhi ya wananchi wanaoishi maeneo yaliyo karibu na hifadhi.

Hatua hiyo inatokana na nguvu kubwa na mashirika ya kiuhifadhi ya ndani na nje ya nchi kujielekeza katika ulinzi wa wanyamapori wakubwa kama tembo, faru, twiga, simba pamoja chui, huku wanyamapori wadogo wakiwindwa kwa kasi na jamii zinazopakana na hifadhi kwa ajili ya kitoweo.

Amewataja wanyamapori hao wadogo wanaowindwa kwa ajili ya kitoweo ni swala, pundamilia, sungura, nguruwepori na digidigi.

Alitoa agizo hilo jana mkoani Arusha alipokuwa akizungumza na watumishi wa kikosi hicho kinachokabiliana na ujangili katika mikoa ya Arusha, Tanga, Kilimanjaro na Manyara.

Akizungumza katika mkutano huo, Kanyasu amesema endapo hatua za makusudi hazitachukuliwa kukabiliana na tatizo hilo, jamii nzima itakuwa hatarini, kwa kuwa wanyamapori kama simba wataanza kuwala binadamu kwa vile wanyama wanaotegemewa kama chakula chao, watakuwa wamekwisha kutokana na ujangili.

Kanyasu alitaja athari zingine ikwamo wanyamapori wakubwa watatoweka kwa kukosa chakula, hivyo sekta ya utalii itaathirika kwa vile kutakuwa na hifadhi zisizo na wanyamapori.

Alisema kufuatia ujangili wa kitoweo kushamiri kwa kasi hata kwa jamii ambazo mwanzo zilikuwa zikiaminika kuwa hazitumii nyamapori ni ishara mbaya katika uhifadhi kwa sababu wanyamapori hao wakubwa ili waweze kuishi, wanategemea uwapo wa wanyamapori wadogo.

Hata hivyo, Kanyasu alizionya jamii hizo kuacha tabia hizo mara moja na kuzitaka ziendelee kuwa rafiki wa uhifadhi.

Aidha, Kanyasu ameitaka KDU kufanya kazi kiweledi kwa kuimarisha mahusiano mazuri na jamii ili kupata taarifa za kiintelijensia kuhusiana na ujangili ukiwa kabla haujafanyika.



Dereva wa guta akiwa amelisheheni mzigo wa magodoro katika eneo la njia panda Kigogo, jijini Dar es Salaam jana, na kumfanya ashindwe kuona vyombo vya moto vinavyokuja nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kinamama wasusi waiangukia serikali

Na Mohab Dominick, KAHAMA

WANAWAKE wanaofanya shughuli mbalimbali za kushona na kusuka nywele katika Wilaya ya Kahama, Mkoa wa Shinyanga, wameomba serikali kuwaondolea kodi wanazotozwa ili wanufaike na kazi zao za mikono.

Wanawake hao wanaomiliki saluni Salome Mvanga na Khadija Shaweji, wakazi wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, walisema kuwa maombi yao wanayaelekeza kwa Rais John Magufuli, ambaye ni mtetezi wa wanyonge.

Walisema changamoto wanazozipata kwa biashara hizo ni bei, na kuongeza kuwa kwa wanawake wanaomiliki saluni wanalipia mapato Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tofauti na mtu anayesukia kibarazani na wa mitaani, wakati wao wanafanya kazi hiyo kwa kutoza gharama ndogo.

"Changamoto kubwa ni bei kwa wanawake, na hii ni changamoto, maana sisi ni tofauti na wale wanaofanya katika maveranda... sisi wenye fremu za pango tunalipa mapato, tuna leseni kwa hiyo bei yetu ni tofauti na wale wa mitaani," alisema Salome.

Alimwomba Rais Magufuli kuangalia changamoto za wanawake hasa wasusi kuwaondolea kodi wanazolipa TRA ama kuwatafutia maeneo yao wanawake wa mitaani wanaosuka nywele ili nao waweze kutambuliwa na serikali na kulipa kodi inayolingana na vipato vyao halisi.

"Hii changamoto inasababisha sisi wanawake kushindwa kupiga hatua za kimaendeleo, tusaidiwe tuna lengo zuri la kuhakikisha na sisi tunapiga hatua za kuunga mkono lengo la kuwa na viwanda vikubwa na vidogo na kufikia uchumi wa kati," alisema Mvanga.

Alisema kuwa wanawake wanaofanya shughuli hizo kiujanja ujanja nao watafutiwe eneo ili kutambulika kwa mujibu wa sheria ili na serikali ipate mapato yake.

## Watu 73 mbaroni tuhuma kuingia nchini kinyemela

Na Manuel Kaminyoge, SONGWE

IDARA ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe imewakamata watu 73 kutoka nchi tisa, wakidaiwa kuwa wahamiaji haramu.

Watu hao walikamatwa Februari, kwa tuhuma za kuingia nchini bila vibali kwa kutumia njia za panya kati ya mpaka wa Zambia na Tanzania pamoja na mpaka wa Malawi na Tanzania.

Kamanda wa Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe, Wilfred William Marwa, alisema watu hao waliokamatwa ni kutoka Somalia, Kenya, Marekani, India, Congo, Burundi, Ethiopia, Zambia na Malawi.

Alisema wahamiaji wengi ni kutoka mataifa jirani ya Zambia na Malawi ambapo Malawi waliokuwa 30, Zambia 19, Congo 6, China 6, Ethiopia 6, Somalia 3, Marekani 1, Burundi 1 na Kenya 3.

Kamanda Marwa aliongeza kuwa kuwapo kwa njia nyingi za panya wanazopitia wahamiaji haramu kunachangia ongezeko, hivyo aliwataka wananchi kutokubali kuwahifadhi watu hao kutokana na kuwapo kwa tishio la ugonjwa hatari wa corona katika nchi mbalimbali duniani.

"Mkoa wetu umepakana na nchi za Malawi na Tanzania. Ni mipaka kwa zaidi ya kilometa 150... iko hali inayopelekea kuwapo kwa njia nyingi za panya," alisema Marwa.

Alisema Idara ya Uhamiaji Mkoa wa Songwe inaendelea na doria katika njia za panya ili kukabiliana na wahamiaji haramu, kwa lengo la kupambana na maambukizi ya virusi vya corona katika mipaka ya Ileje na Tunduma.

Abubakali Ally, mkazi mkoa wa Songwe alisema kuwa kutokana na kuwapo kwa njia nyingi za panya zinazopelekea wahamiaji haramu wengi kupita humo, serikali iweke sheria kali na zenye adhabu kubwa kwa watakaobainika wanatumika kuwaficha na kuwasafirisha wahamiaji haramu.

Michael Swila, mkazi wa Wilaya ya Momba mkoani Songwe, alisema kuwa kuwapo kwa mwingiliano mkubwa wa watu katika mpaka wa Tunduma, serikali ingesitisha kwa muda baadhi ya shughuli mpakani hasa katika kipindi hiki ambacho kila nchi inachukua tahadhari kubwa dhidi ya ugonjwa wa corona.



Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Biashara na Haki za Binadamu Tanzania (BRHT), Wakili Flaviana Charles, akizungumza katika mkutano wa wadau wa biashara na haki za binadamu, uliofanyika jijini Dar es Salaam juzi, na kuhimiza uwekezaji unaozingatia haki za binadamu. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TCCIA yatoa neno biashara mlipuko virusi vya corona

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

CHEMBA ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima nchini (TCCIA), imewataka wanachama wake wanaofanya biashara za dawa ya kunawia mikono (hand sanitizers) na visiba mdomo (masks) vinavyotumika kujikinga na virusi vya corona, waingiwe na moyo wa huruma kwa wananchi wenzao kwa kutopandisha bei ya bidhaa hizo.

Rais wa TCCIA, Paul Koyi, alitoa rai hiyo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wadau mbalimbali wakiwamo viongozi serikalini kuhusiana na tabia iliyojitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara kupandisha bei za bidhaa hizo kwa asilimia 30 hadi 50 katika maeneo mbalimbali nchini muda mfupi baada ya serikali kutoa taarifa iliyothibitisha kuingia kwa ugonjwa nchini.

"Kwa niaba ya Bodi ya TCCIA, kwanza tupeane pole kwa janga hili la ugonjwa wa corona ambalo limeingia nchini kwetu. Ugonjwa huu ni adui wa kiuchumi kwa kiasi kikubwa mno kama ambavyo tumekwishaona kwenye nchi za wenzetu na sasa hapa kwetu," alisema kiongozi huyo ambaye kwa sasa yuko katika ziara ya kikazi Nyanda za Juu Kusini.

Aliwaomba wanachama watimize wajibu wao kwa kuwauzia wananchi bidhaa hizo kwa bei halali na elekezi bila kusahau kuzingatia ubora.

Taarifa za kuwapo kwa ugonjwa wa corona nchini zilithibitishwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika mkutano wake na waandishi wa habari.

Waziri huyo alitangaza kuwa Mtanzania aligundulika na maambukizo ya virusi hivyo baada ya kurejea nchini akitokea Ubelgiji kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

Juzi, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kuwa idadi ya wagonjwa imeongezeka nchini na kufikia watatu na serikali imechukua hatua mbalimbali za kudhibiti maambukizo hayo ikiwamo kufunga shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu na kukataza mikusanyiko ya watu.

"TCCIA inapenda pia kutoa pole ya dhati kwa serikali yetu na kuipa moyo kuendelea na juhudi za kupambana na ugonjwa huu. Kwa kuwa taasisi yetu ya TCCIA ni ya kibiashara na kiuchumi kwa asilimia mia moja, nawaomba wanachama wetu wote popote mlipo kuwa njia pekee itakayotuokoa kuepukana na hasara kubwa za kibiashara na kiuchumi, ni kuzingatia hatua za kujikinga kwani kinga ni bora kuliko tiba.

"Tufuate taratibu za wataalamu wetu wa afya na maelekezo yote muhimu yanayotolewa katika kupigana na ugonjwa huu," Koyi alisema.

## Watumishi h/shauri kuelimishwa corona

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WATUMISHI wa Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara, wanatarajia kupatiwa elimu ya namna ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona ili elimu hiyo waweze kuifikikisha kwa jamii wanayoihudumia katika sehemu zao za kazi.

Hayo yalielezwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Masasi Mkomaindo, Dk. Salum Gembe, alipokuwa akielezea njia za kujikinga na ugonjwa wa corona katika kikao maalumu na mkuu wa wilaya hiyo, Selemani Mzee, kilichofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ambapo wadau mbalimbali wa maendeleo pia walishiriki.

Dk. Gembe alisema wameamua mkakati huo wa kutaka kutoa elimu kupitia watumishi wote wa idara zote ili kupanua wigo mpana katika kufikisha elimu ya kujikinga na ugonjwa huo.

Alisema uamuzi wa kutaka kutoa elimu kwa watumishi wa idara zote za halmashauri hiyo unalenga kuona elimu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona inaifikia jamii kwa mapana zaidi.

Alisema iwapo kila mtumishi atakuwa na elimu ya kutosha, itakuwa rahisi pia kwa wananchi wengine kupata elimu hiyo na kuzingatia kujikinga kwa sababu watumishi wanakutana na wananchi wengi kwenye sehemu zao za kazi.

"Mkakati wetu katika kuhakikisha elimu ya kujikinga na virusi vya corona inafika kwa jamii...tutatoa elimu kwa watumishi wa halmashauri na tutalifikia kila kundi katika kutoa elimu hii lengo jamii ya Masasi kuwa na uwelewa wa kutosha katika kujikinga na corona," alisema Dk. Gembe.

Alisema watumishi wanatakiwa kuwa mfano katika maeneo ya kazi kwa kuhakikisha kila ofisi inakuwa salama kwa kuweka vyombo vya kunawia maji mikono kabla ya kutoa huduma kwa mwananchi, na anayehudumiwa pia kuzingatia hilo kabla ya kuingia kuhudumiwa.

# Wafanyabiashara watakiwa kuzingatia umuhimu afya

**Na Mary Geofrey**

JUMUIYA ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT), imewataka wafanyabiashara kuzingatia umuhimu wa afya na nguvu kazi ya taifa na unyeti wa biashara nchini kiuchumi wakati ambao nchi ipo kwenye janga la maambukizi ya virusi vya corona.

Jumuiya hiyo, imewataka kuhakikisha kila eneo la wafanyabiashara linawekwa kemikali muhimu maji tiba kwa ajili ya wateja na wauzaji wa eneo husika pamoja na karatasi nyeupe za kujikaushia.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa JWT, Stephen Chamle, ilieleza kuwa wafanyabiashara waendelee kufanya biashara hadi hapo watakapopata uamuzi mwingine kutoka serikalini.

Alisema ikilazimu wafanyabiashara watumie vifaa vya kujikinga kama maski ili kuepuka kuendelea kueneza virusi hivyo kwenye mikusanyiko.

Chamle alisema pia kila mfanyabiashara anapaswa achukue tahadhari azionapo dalili zozote za wateja awashauri kufika kituo cha afya au kupiga simu bure kwa namba 0800110124 au 0800110125.

Alisema ni vizuri kwa kutegemea eneo la biashara, kila mmoja awe na maji kwenye kifaa maalumu kwa ajili ya usafi wa mara kwa mara.

"Kwa kuzingatia hali ya biashara hasa baada ya mlipuko huu wa virusi vya corona, jumuiya inaendelea kujipanga kuchukua juhudi mbalimbali za kuomba serikali kupitia taasisi mbalimbali zinazo walenga wafanyabiashara kutazama upya anguko la biashara na njia ya kumsaidia katika kipindi hiki cha mpito ambacho ni maombi ya ulimwengu, janga hili liishe na kufika tamati," alisema Chamle.

Aliwataka wafanyabiashara kuwa watulivu hasa kipindi hiki kigumu ambacho serikali inaendelea kuchukua juhudi kadhaa kwa kuamini matokeo ya kupungua kwa maambukizi huko China ambako mlipuko ulianzia na kuliponya taifa.

# DED azuia minada kisa corona

**Na Allan Isack,** BABATI

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Babati, Hamisi Malinga, amezuia kufanyika biashara katika mnada maarufu wa Maole, kijiji cha Maweni Kata ya Magara mkoani Manyara.

Kuzuiwa biashara kwenye mnada huo, kumetokana na agizo la serikali kupiga marufuku mikusanyiko ya watu.

Malinga alisema kutokana na agizo la Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, wameanza kutekeleza. Alisema juzi majira ya asubuhi alitoa tangazo wafanyabiashara wote kusambaratika katika eneo la mnada wanapofanyia biashara mbalimbali kwa kuwa serikali imepiga marufuku mikusanyiko.

Aliwataka wafanyabiashara hao kutii agizo la serikali na kujali utu na ubinadamu kuliko kuthamini biashara zao.

Aliwataka wafanyabiashara kuwa na subira hadi hapo hali ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona itakapokuwa nzuri ndipo wataruhusiwa kuendelea na biashara.

Alisema anatambua kuwa mnada huo ni chanzo cha mapato kwa serikali na Halmashauri ya Wilaya ya Babati, lakini afya na maisha ya watu ni muhimu kuliko mapato.

Katika mnada huo, kulizuka taharuki ambapo iliwalazimu mgambo kufika katika soko hilo, na kutumia nguvu kuwaondoa wafanyabiashara.

Mnada huo hufanyika kila Jumatano na huwakutanisha wafanyabiashara kutoka mikoa ya Arusha na Manyara.

Serikali ilisitisha mikusanyiko yote mikubwa ya ndani isiyo ya lazima, zikiwamo shughuli za michezo, matamasha ya muziki, mikutano ya kisiasa, mahafali na kufungwa kwa shule za msingi, sekondari na vyuo vyote nchini.

Pia Waziri Mkuu aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya, kuhakikisha kuwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wagonjwa wa maambukizi ya ugonjwa wa corona wanatoa huduma ipasavyo.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (wa pili kushoto), akiangalia pikipiki zilizokamatwa na Kikosi Dhidi ya Ujangili (KDU), Kanda ya Kaskazini kinachoshughulikia mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara, alipotembelea makao makuu ya kikosi hicho, jijini Arusha jana, kabla ya kuzungumza na watumishi. **PICHA: WMU**

# Wachimbaji wa Tanzanite watakiwa tahadhari corona

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WACHIMBAJI wa madini wa Mkoa wa Manyara, wametakiwa kuchukua tahadhari ya ugonjwa wa corona.

Wametakiwa kufuata maagizo ya serikali ya kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, kunawa mikono kila mara kwa maji yanayotiririka na kuvaa barakoa hata nje ya migodi yao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini mkoani Manyara (Marema), Justin Nyari, aliyasema hayo wakati akizungumzia mikakati ya kupambana na maambukizi ya ugonjwa wa corona kwa wachimbaji madini wa eneo hilo. Nyari alisema wachimbaji hawanabudi kuchukua tahadhari ya maambukizi ya ugonjwa huo, kwa kutimiza maagizo ya serikali yaliyotolewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu. Alisema japokuwa wachimbaji madini wanavaa vifaa vya barakoa kujikinga na vumbi na hewa chafu wakiwa ndani ya mgodi, lakini kwa sasa wanapaswa kuvaa hata nje ya migodi.

Pia alisema tahadhari za afya zinapaswa kuchukuliwa kwa maeneo ya machimbo ukiwamo usafi kwa wachimbaji kunawa mikono kwa maji yanayotiririka na sabuni kwenye maeneo yote migodini na kwenye migahawa.

"Kama tukiona kuna mtu mwenye dalili za mafua makali, kuumwa kichwani, kushindwa kupumua, tunaomba tutoe taarifa kwa mamlaka husika kwenye eneo la jirani," alisema.

Alisema maagizo ya serikali ya kunawa kila mara yanapaswa kutekelezwa kwenye kila mgodi kuweka maji na sabuni mlangoni ili watu wote wanaoingia na wanaotoka migodini kunawa mikono kila wakati.

Mmoja wa wachimbaji wa madini ya Tanzanite wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, Hassan Juma, alisema wachimbaji wanapaswa kuchukua tahadhari zinazotolewa na viongozi wa serikali.

Alisema hadi sasa hakuna taarifa ya mchimbaji madini kuwa na maambukizi ya virusi vya corona, lakini wanatakiwa kuchukua tahadhari kwa kufuata maelekezo yanayotolewa.

"Hatupaswi kusubiri mtu mwenye corona aonekane migodini na serikali ifunge migodi, tuchukue tahadhari ili ugonjwa usiingie, na serikali isisitishe uchimbaji kwa kuwa tutakufa njaa, tuwe makini tusiruhusu maambukizi kwenye uchimbaji," alisema.

# Wapewa mafunzo kukabili majanga

**Na Allan Isack,** MANYARA

KAMATI ya maafa ya Mkoa wa Manyara, wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na majanga yanayotokea mkoani humo.

Mafunzo hayo yalitolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, ili kukabiliana na maafa mbalimbali yanayotokea nchi.

Hivi karibuni Mkoa wa Manyara ulikumbwa na majanga kadhaa ikiwamo watu kufa kutokana na mafuriko yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha, mazao kuzolewa na maji, nyumba kusombwa na maji, pamoja na watu kujeruhiwa baada ya nyumba kuezuliwa na upepo mkali.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Missaile Mussa, akizungumza Mjini Babati juzi wakati wa kufungua mafunzo hayo, aliwataka washiriki kuzingatia maelekezo yote watakayofundishwa.

Alisema washiriki hao watauwakilisha vyema Mkoa huo kwenye mafunzo hayo.

Alisema baada ya mafunzo hayo, anatarajia washiriki watayatumia kuielimisha jamii.

Washiriki watajengewa uwezo wa kupambana na matatizo mbalimbali yanayojitokeza kwenye jamii.

"Nawashauri washiriki mafunzo haya mfuatilie kwa makini, ili mkayatumie kutoa elimu kwa jamii juu ya namna ya kukabiliana na majanga yanayotokea," alisema Mussa.

Mratibu wa Maafa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Harrison Chinyuka, wakati akiwasilisha mada ya mafunzo hayo, alisema mafunzo hayo yataleta matokea chanya kwenye jamii kupitia kwa kuwatumia washiriki hao.

Alisema kamati hiyo imeshatoa mafunzo kwa kamati za wilaya, halmashauri, kata hadi kwenye jamii namna ya kujikinga na majanga.

Aidha, alisema kujikinga na maafa na majanga kunapunguza gharama kuliko kudhibiti.

"Kila idara pamoja na wananchi wana jukumu la kupambana na maafa, tukitoa elimu kwa kiwango cha hali ya juu tutapunguza kwa kiasi kikubwa," alisema Chinyuka.

Kamati ya Maafa ya Mkoa huo, inaundwa na wakuu wa vitengo, viongozi wa dini, wazee wa mila, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Chama cha Msalaba Mwekundu na vyama vya siasa.

Mafunzo hayo yametolewa kwa siku mbili Mjini Babati kwa udhamini wa Chama cha Msalaba Mwekundu Tanzania.



# TRA yakamata magunia 13 ya kondomu

**Na Mary Mosha,** ROMBO

MAMLAKA ya Mapato Mkoa wa Kilimanjaro (TRA), imekamata mipira ya kiume (kondomu) magunia 13 yenye uzito wa kilogramu 578.6 zilizoingizwa nchini kwa njia zisizo rasmi (njia za panya) kutoka nchini Kenya, kwenda jijini Dar es Salaam.

Akizungumzia tukio hilo Meneja wa Mamlaka hiyo Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi alisema, bidhaa hizo ziliingizwa nchini Machi 15, mwaka huu na zilipakizwa katika basi kituo cha Tarakea, wilayani Rombo kwa kusafirishwa.

Mwangosi alisema, mipira hiyo inaonyesha kuwa ilinunuliwa na Serikali ya Kenya kwa ajili ya kutumika na watumishi wa serikali hiyo na iliingizwa nchini kwa njia zisizo rasmi na kudai kuwa kwa sasa wamebaini wafanyabiashara wasio wazalendo wanaingiza bidhaa za magendo na kuzisafirisha kwa kutumia mabasi ya abiria.

"Baada ya kuweka juhudi kubwa katika kuhakikisha tunakomesha biashara za magendo sasa hivi tumebaini wafanyabiashara wasio waaminifu wamebuni njia ya kusafirisha bidhaa zao kwa kutumia mabasi ya abiria wakijua fika hatutakuwa tukiyakagua mabasi hayo, hili wanajidanganya ni bora wakaacha kabisa biashara hii na wakafuate sheria katika kuingiza mizigo yao," alisema Mwangosi. Alisema, changamoto wanayokabiliana nayo katika ukaguzi wa mabasi ya abiria ni baadhi ya abiria wamekuwa wakilalamika kucheleweshwa safari zao na kutumia nafasi hiyo kuwaasa wenye mabasi hasa yanayotokea wilayani Rombo kuhakikisha abiria mwenye mizigo mikubwa wana nyaraka halali pamoja na viambatanishi vyote vinavyoonyesha amelipia gharama za usafirishaji.

"Wamiliki wa magari ya abiria mkiwa na wasiwasi wa nyaraka ambazo amekuonyesha abiria mwenye mzigo toa taarifa kwetu kabla ya kuanza safari ili kuepuka usumbufu kwa abiria wawapo njiani," alisema Mwangosi.

Meneja msaidizi wa mkoa anayehusika na masuala ya forodha, Edwin Iwato, alisema serikali iliviondolea kodi vifaa tiba vyote vinavyoingizwa nchini, lakini iliweka sheria na hatua za kufuatwa kabla ya kuingizwa nchini ikiwamo kukagua ubora wa vifaa hivyo, lakini kwa mipira hiyo hazikifuata sheria.

Iwato alisema, changamoto kubwa ni wananchi wanaoishi eneo la mpakani kujihusisha na biashara za magendo. Alisema wanatoa elimu kwa wananchi kuachana na biashara hiyo na wanaokiuka watachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Mwananchi aliyekuwa akisafirisha bidhaa hizo, Stella Yusuph, alisema alienda Nairobi nchini Kenya kwa ajili ya semina kwa waathirika wa virusi vya Ukimwi na baada ya semina hiyo alipewa mipira hiyo kuja nayo Tanzania kuwapatia bure waathirika wa Ukimwi waliopo katika vikundi maalum jijini Dar es Salaam.

Yusuph, alisema biashara hiyo ya kuingiza mipira hiyo nchini huifanya mara mbili kila mwaka na juzi ilikuwa mara yake ya tatu tangu aanze.



Wakazi wa Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, wakivua samaki pembeni ya barabara ya Kairo-Zaire, baada ya mafuriko yaliyotokana na bwawa la Kidawash kujaa maji, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kibong'oto yajipanga kupambana corona

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WAKATI makali ya virusi vya ugonjwa wa corona yakizidi kung'ata, Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto (KIDH), imesema hivi sasa inaandaa kikosi kazi cha wanasayansi wa kimataifa kitakachobuni, kupanga, kutekeleza na kutathmini mikakati ya kudhibiti na kukinga magonjwa ambukizi nchini.

Taarifa ya Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Riziki Kisonga, iliyokabidhiwa kwa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, baada ya Waziri Mkuu kusitisha mikusanyiko, semina na kuzifunga shule zote na vyuo, inaeleza kuwa kikosi kazi hicho kinajumuisha wanasayansi wenye shahada ya uzamivu.

"Kazi tuliyonayo kwa sasa ni kuandaa world class medical experts and scientists (kikosi kazi cha wataalamu wa utabibu na wanasayansi wa kimataifa) wapatao watano wenye shahada za uzamivu, wanane wenye shahada za uzamili, na mmoja ambaye ni mtaalamu wa kimataifa katika viwanda vya vifaa," imeeleza taarifa hiyo.

Pia, hospitali hiyo imetangaza kuanza ushirikiano na baadhi ya vyuo vikuu vilivyopo Marekani kama Virginia na Califonia, San Franscisco katika tiba, mafunzo na tafiti za kifua kikuu sugu zaidi (MDR-TB).

Hospitali hiyo pia, inashirikiana na nchi za Ulaya katika mafunzo na utafiti, vyuo hivyo ni Liverpool, St. Andrews (Uingereza), Munich-LMU (Ujerumani), Radboud (Uholanzi), Copenhagen (Denmark), MDR-TB Training Centre-Riga (Lativa) na LHL International (Norway).

Kuhusu changamoto zinazoikabili hospitali hiyo, Dk. Kisonga, alisema Kibong'oto haina muundo na mfumo wa uendeshaji ambao unaakisi kazi nyingi za utoaji huduma wa kibingwa (rufani), mafunzo ambayo yameendelea hasa kwa kuanza na watumishi wa ndani ya nchi pamoja na ufanyaji tafiti na jukumu jingine la kufuatilia mwenendo wa vimelea vya magonjwa ambukizi na hatarishi ya mlipuko.

"Kwa sasa kuna hatua ambazo zimeshachukuliwa kwa wizara kutengeneza muundo wa hospitali, na kimsingi andiko la mabadiliko ya Hospitali ya Kibong'oto kuwa Taasisi ya Afya ya Jamii na Magonjwa Ambukizi Kibong'oto linaendelea kukamilishwa. Lengo lake ni kupata sheria itakayoanzisha taasisi hiyo," imefafanua taarifa hiyo.

# Mlipuko ugonjwa wa miche watafutiwa ufumbuzi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

SERIKALI imeahidi kutafuta ufumbuzi wa mlipuko wa ugonjwa mbaya unaoshambulia miche inayotokana na miti ya kupandwa katika Shamba la Miti la Taifa la West Kilimanjaro, lililopo Wilaya ya Siha.

Kwa mujibu wa wataalamu wa wizara hiyo, ugonjwa huo uliolipuka wa kuozesha miti unafahamika kama 'dumping off'.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasa, aliahidi hayo juzi wilayani hapa, baada ya kukagua shamba la miti la West Kilimanjaro lililopo chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).


Kabla ya serikali kutoa ahadi hiyo, msimamizi wa bustani ya miche katika shamba hilo, Devota Bura, alimweleza Naibu Waziri huyo kuna kila sababu ya wizara husika kutafuta majibu ya kisayansi ya chanzo cha ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa Bura, ugonjwa huo huathiri zaidi shina la miche, huoza na hauendelei kukua na kufa.

Alisema ugonjwa huo huanza katika kitalu cha miche na hatimye huamia kwenye viriba.

"Unaweza kuotesha miche 50,000 ikakua miche 35,000, huku 15,000 yote ikawa imeshambuliwa na ugonjwa huo na kufa. Tumejitahidi kupiga dawa, lakini imeonekana bado ugonjwa huu unashambulia miche, hali ambayo inasababisha kutofikia malengo tunayokuwa tumejiwekea kwa mwaka mzima," alieleza Bura.

Kanyasu alisema ataagiza wataalamu wa idara ya utafiti kuchunguza ugonjwa huo na kisha serikali itatoa mwongozo wa namna ya kukabiliana na ugonjwa huo.



Ukurasa 20

Tuzo za Tehama kwa waimarishaji biashara katika sekta mawasiliano



Ukurasa 16

Mradi WIN na mkakati unaowasogeza kinamama wanahabari mtaa '50/50'




Ukurasa 14

## Daraja Namba Sita Afrika linalotarajiwa kuleta uchumi, maisha mpya Kanda ya Ziwa

BUFE

IJUMAA MACHI 20, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



# Ewura walivyopania mwisho wa 'vishoka' umeme Nyanda za Juu

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

WAKATI serikali sasa inalenga takriban umeme kwa kila nyumba nchini ifikapo mwaka 2021, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, iko katika mpango endelevu wa kukabiliana na vishoka waunganishaji umeme majumbani bila ya leseni.

Ewura katika lengo hilo, inanuia kukabili wimbi la mafundi wabaishaji maarufu kama 'vishoka'ili kuepusha hatari, ikiwamo nyumba kuungua au kupata hitilafu za umeme kila mara, sababu kuu ni uunganishaji usiozingatia utaalamu kutoka kwa 'vishoka.'

Sheria ya Umeme nchini zinazosimamia shughuli za Tanesco na Ewura, zinaweka wazi kwamba ni makosa mtu kuunganisha mifumo ya umeme bila ya kuwa na leseni kutoka Ewura, inayotambulisha kufanya kazi katika jamii.

INAENDELEA UK.18

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## Vita vya corona: Njia 5 kufanya kazi nyumbani Ukurasa 15

BIASHARA

# Daraja Namba 6 Afrika linalotarajiwa kuleta uchumi mpya Kanda ya Ziwa



Rais Dk. John Magufuli, alipoelekeza jambo katika uzinduzi wa ujenzi wa Daraja la Kigongo Busisi, Desemba mwaka jana, ambayo picha yake itakavyomalizika inaonekana. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

NI safari ambayo serikali inaendelea nayo katika kusaka maendeleo ya uchumi, katika upande wa ujenzi wa miundombinu, eneo ambako Rais Dk. John Magufuli, ametumikia kwa muda mrefu katika nafasi yа uwaziri.

Miundombinu, inagusa barabara nyingi za kiwango cha lami na madaraja, vyote vikiwa nyenzo muhimu kufikia Uchumi wa Kati unaolengwa ifikapo mwaka 2025, ambao kimsingi unatawaliwa na ustawi wa viwanda,

Chini ya kaulimbiu inayotawala 'hapa kazi tu' umeendeleza kazi zilizotangulia katika zama zilizopita za uongozi kama vile ujenzi wa barabara zenye madaraja yaliyokomboa mfumo wa usafiri.

Mifano hai inajumuisha Daraja la Mkapa, lililopo Rufiji katika barabara kuu ya Dar es Salaam - Mtwara ambalo zamani uvukaji wake palitumika pantoni na Daraja la Umoja, linalounganisha Mtwara-Tanzania na Msumbiji, pia Daraja la Kikwete, linalovuka Mto Malagarasi, mkoani Kigoma.

Pia, kuna miundombiniu nyinginezo mpya ambazo Rais Dk. Magufuli anazitumikia hadi sasa kama vile uboreshaji wa reli iliyopo na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR), uanzishaji hifadhi mpya na kuboresha hifadhi za taifa, sekta ya madini pamoja na uvuvi.

Unaporejewa mkoa na jiji la Mwanza, sehemu ya manufaa lliyowafikia wananchi wake na Kanda ya Ziwa kwa jumla, ni kujengwa daraja la Kigogo- Busisi iliyozinduliwa mwaka jana, kwa kuwekewa jiwe la Msingi na Rais Dk. John Magufuli.

> “Litachochea uzalishaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwemo kilimo, ufugaji, biashara, uvuvi na utalii ambalo litakuwa kiungo cha mikoa ya Kanda ya Ziwa; Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera na Kigoma.



Ni daraja litakalojengwa katika kivuko hicho kilichoko kwenye Ziwa Victoria ni kubwa kulinganisha na madaraja yote ya Afrika Mashariki na la sita katika nchi za Afrika.

**WAZIRI KAMWELWE**

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, anaeleza namna litakavyokuwa na manufaa mengi ya kiuchumi kwa wananchi wa maeneo jirani na mikoa ya mbali, ikiwamo katika biashara.

Ni mradi wa daraja lenye urefu wa kilomita 3.2 na upana wa mita 28.45, ambalo ujenzi wake unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 699.2, Waziri akisema ujenzi wake unatarajiwa kuchukua miezi 48 (miaka minne), likiwa na nguzo 67.

"Litakuwa na njia nne, hivyo likikamilika wananchi, magari yatatumia dakika nne tu kuvuka,' anasema Waziri Kamwelwe na kufafanua kwamba, hali iliyopo sasa, magari ya wavukaji baadhi yenye mizigo, wanalazimika kutumia muda kati ya saa moja hadi saa mbili na nusu.

Anataja madaraja makubwa matano ya Afrika kuwa ni, la kwanza liko nchini Misri (Setro Oktobar) lenye urefu wa kilomita 20.5 na la pili liko nchini Nigeria, lenye urefu wa kilomita 11.

Pia, kuna la tatu linalouvuka Mto Suez Canal nchini Misri, lenye




Mtendaji Mkuu Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Patrick Mfugale na Mwakilishi kutoka kampuni ya ujenzi ya China Civil Engeering Construction Coorporation, Zhang Jang, wakionyesha nakala za mkataba wa ujenzi wa Daraja la Kigongo- Busisi .

mwaka 2014/2015, lakini wafadhili walipoona ukubwa wa mradi wenyewe wa waligeuka nyuma.

Rais Dk. John Magufuli, ambaye ni mzoefu zaidi katika wizara inayohusika na muiundombinu, alipoingia madarakani aliiagiza Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) kuanza usanifu wa ujenzi kupitia kampuni ya Kichina, kazi iliyokamilika mwaka 2018, ikitoa bajeti ta Sh. bilioni 2.8.

Katika uzinduzi wa mradi, Dk. Magufuli alifafanua utekelezaji wake kwa kauli: "Hatujaomba mkopo, wala hatujampigia magoti mtu atupe fedha. Tunajenga kwa fedha zetu wenyewe za makusanyo ya kodi za wananchi."

Ni daraja linalotarajiwa kuiunganisha Mwanza na Geita na barabara zake katika ukanda wa Ziwa Victoria, pia barabara kuu ya Shinyanga, Kigoma, Kagera na nchi jiraji za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC)

**KWA NINI INAJENGWA?**

Waziri Kamwelwe anafafanua ujenzi huo ni wa kuwaondolea wananchi kero za kivuko na kuimarisha ulinzi na usalama wa mizigo na usafiri wa abiria kuzama kwenye vivuko kila mara, sambamba na kuwarahisishia uchukuzi na usafirishaji wa magari, abiria na mizigo.

"Malengo mengine ni kukuza na kuchochea uzalishaji katika sekta za uvuvi,madini,viwanda pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano wa kibiashara ndani na nje katika nchi za Rwanda, Uganda,Burundi pamoja na demokrasia ya Congo(DRC)," Mhandisi Kamwelwe.

Pia, anasema ni utekelezaji wa maono ya kiserikali, barabara kuu zote zinazounganisha makao makuu ya wilaya zijengwaekwa kiwango cha lami, ili zipitike kirahisi majira yote.

Hivyo, daraja hilo kujengwa linaingia katika orodha ya madaraja 8,020 yaliyopo nchini, kati yake makubwa ni 77.

> **"Daraja likikamilika, wananchi watatengeneza fedha. Wale nyumba zao zitabomolewa kupisha ujenzi huo watalipwa. Serikali imetenga Sh.bilioni 3.45, lakini ni wale tu watakaostahili.**

**KAULI YA UZINDUZI**

Wakati wa kuzindua ujenzi w a daraja hilo na kuweka jiwe la msingi, Rais Dk. John Magufuli, aliahidi litakapokamilika, litakuwa fursa kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na nchi jirani.

"Litachochea uzalishaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, ikiwemo kilimo, ufugaji, biashara, uvuvi na utalii ambalo litakuwa kiungo cha mikoa ya Kanda ya Ziwa; Mwanza, Shinyanga, Geita, Kagera na Kigoma," alisema, huku akitaja wa nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda, Kenya na DRC kuwa wanufaika.

Kwa mujibu wa Rais, daraja hilo ni mwendelezo wa kutimiza ahadi zake katika kampeni za uchaguzi mkuu uliopita, kuhusu miradi mbalimbali ya maendeleo nchini.

"Daraja likikamilika, wananchi watatengeneza fedha. Wale nyumba zao zitabomolewa kupisha ujenzi huo watalipwa. Serikali imetenga Sh.bilioni 3.45, lakini ni wale tu watakaostahili," aliahidi Dk. Magufuli.

Mtazamo wake ni kwamba, mradi utaleta manufaa makubwa kwa Watanzania, huku akibashiri uzalishaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi, ikiwamo uvuvi katika Ziwa Victoria utakuwa maradufu.


Wito wa Rais Magufuli ni kwamba, mradi huo unatakiwa kukamilika kwa wakati,makandarasi wasimamie hizo fedha za Watanzania zipo za kutosha wafanye kazi usiku na mchana,badala ya kuwachelewesha huduma wananchi.

Pia, Rais Dk. Magufuli anawaomba wananchi kuitunza daraja hilo na kuchangamkia fursa zitokanazo na kukamilika lenye, akidokeza fursa za ajira na biashara.

Anawataka wananchi kufanya kazi kwa bidii, kuleta heshima ya nchi na wasisubiri vifaa vya ujenzi, kwani ni tendo la kuwaibia Watanzania wote walipa kodi na wenye maisha ya chini.

***Mwandishi wa makala hii anapatikana kwa anwani ya barua pepe: anthonygervas@yahoo.com na simu(+225)0682 86 92 44, Kanda ya Ziwa.***

# Vita vya corona: Njia 5 kufanya kazi nyumbani



Mtu akifanya kazi kutoka nyumbani. **PICHA: MTANDAO**

INAELEZWA hadi sasa duniani kuna watu takribani milioni 1.5 wanaofanya kazi nyumbani. Sasa kuna janga la mlipuko wa ugonjwa wa corona. Kazi zinazowezekana kufanyika nyumbani, zifanywaje?

1. Uvaaji nguo; hali ya kuvaa nguo za kulalia siku nzima ni kitu kinachosukuma hamu ya kufanya kazi kutokea nyumbani. Pia, kuna suala la kuoga ambayo kisaikolojia inatoa msukumo kujiandaa kuanza kufanya kazi.

Baadhi ya watu wanaona kuvaa mavazi rasmi ya kazi wakiwa nyumbani, inawasaidia, hasa kama wanataka kupiga simu za kikazi za video.

Hivyo, kuvaa mavazi ya heshima wakati wa kufanya kazi za ofisini ukiwa nyumbani, kunainua ari ya kutoka nyumbani, kuufanya ubongo kuelewa kuwa siku ya kazi zimekwisha.

2. Kuweka mipaka; ikiwa mtu ameajiriwa, ni wazi umeweka saa kadhaa za kazi na muhimu kuzingatia hilo ikiwa utakuwa unafanya kazi kutokea nyumbani. Kuwa tayari kuanza siku yako muda ule ule kama utakaokuwa umewasili ofisini au mahali pa kazi na maliza siku yako muda uleule unaokuwa mahali pako pa kazi.

Mwanablogu, Em Sheldon na mwandishi wa kujitegemea, anasema huwa anafuata ratiba hiyo hiyo hata akifanyia kazi nyumbani anashauri " kulala kwa muda unaofaa ili upate usingizi wa kutosha kwa ajili ya kuamka kwa muda unaofaa siku inayofuata. Mwisho wa siku ya kufanya kazi, ni bora kuzima kompyuta yako na kuondoa karatasi na vitu vingine. Nafasi inayoruhusu, tenga eneo maalum, tofauti katika nyumba yako ambapo unaweza kujiwekea dawati sawa na eneo lako la kazi.

Kama kuna watu wengine nyumbani, kutafuta nafasi ambayo si rahisi kusumbuliwa ni muhimu.

3. Toka nje utembee (kama haujajiweka karantini); Kufanya kazi nyumbani haimaanishi kujifungia siku nzima. Si vibaya kutoka ndani ya nyumba angalau mara moja kwa siku.

Hivyo, vaa viatu vyako, toka nje na furahia hewa safi. Hali hiyo inasaidia kukupa mawazo mapya au namna nyingine ya kushughulikia jambo lililokuwa likikupa ugumu.

Ikiwa huwezi kwenda nje, unaweza hata kuleta mazingira ya ofisi nyumbani kwako.

4. Pokea simu; Kama unafanya kazi kutoka nyumbani, kuna uwezekano utakuwa peke yako, hivyo hautasumbuliwa na wafanyakazi wenzako na mazungumzo au kelele nyingine za ofisi.

Unapokuwa kazini, kuna uwezekano wa mazungmzo na wenzako, lakini ukifanya kutokea nyumbani, utatumia siku nzima bila kuzungumza na mtu yeyote, hali inayoweza kuwa kama kujitenga.

Pata muda wa kupokea simu, uwe na mazungumzo, kuliko kutegemea barua pepe au ujumbe wa papo kwa hapo.

5. Jipumzishe mara kadhaa; Ni vizuri kuwa na utaratibu unapofanya kazi kutokea nyumbani kupumzika, isiwe kung'ang'ania kufanya kazi mfululizo.

Usigande kwenye kompyuta yako siku nzima. Ni muhimu kujipumzisha kidogo kuyaondoa macho yako kutoka kwenye kioo cha kompyuta na kunyanyuka kutoka kwenye kiti chako, unatembea kidogo kama ambavyo ungefanya ofisini.

Utafiti pia umebaini kuwa, mapumziko mafupi kadhaa siku nzima, yana faida kuliko kuwa na mapumziko marefu baada ya muda mrefu.

Ellie Wilson, ni mwanzilishi wa kampuni ya Virtalent, yenye wafanyakazi zaidi ya 50 wanaofanya kazi wakiwa nyumbani anafafanua: "Ni muhimu kunyanyuka na kujinyoosha, kutembea tembea hata kutoka nje na kutembea kujipumzisha na kazi za kwenye kompyuta yako. **BBC**

UCHUMI

# Mradi WIN na mkakati unaowasogeza kinamama wanahabari mtaa '50/50'



Meneja wa Kujengea Uwezo kwa nchi za Afrika katika mradi wa WIN, Jane Godia, akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari wanawake waliohudhuria mafunzo hayo mwaka huu. Chini, waandishi wa habari wakisikiliza kwa makini mafunzo yanayoendelea. **PICHA ZOTE :JENIFER GILLA**

**Na jenifer Gilla**

KILA inapofika Machi ya mwaka, huadhimishwa Siku ya Wanawake Duniani. Ni mahsusi kutambua thamani ya mwanamke katika jamii.

Ikiwa inatimiza miaka 107 mwaka huu tangu kuanza kuadhimishwa kwake inasherehekewa ikiwa na kaulimbiu 'Usawa kwa wote" ikimaanisha kuwapo usawa kati ya mwanamke na mwanamume.

Katika kutekeleza azma hiyo, taasisi mbalimbali zinajitokeza kila siku kumuwezesha mwanamke ajitambue na kujithamini, ili aweze kupigania haki yake ya usawa katika idara mbalimbali, kama ilivyo kwa mwanaume.

Kuna shirika la kimataifa linalopambana kuhakikisha mwanamke anapata nafasi ya juu katika uongozi, linaloitwa The World Association of Newspaper and News Publishers (WAN IFRA), kupitia programu yake inayolenga kuwainua kinamama katika fursa za uongozi liitwalo Women in News (WIN). Wan Ifra kila mwaka, inatoa mafunzo kwa waandishi wa habari wanawake kutoka nchi 15 za Afrika.

Lengo ni kuwapa ujuzi utakaowawezesha kukuza taaluma zao na kuwapatia fursa ya kupanda vyeo katika taasisi wanazotumikia kikazi.

Jane Godia, ni Meneja wa Kujengea Uwezo kwa nchi za Afrika katika program hiyo, anasema wanatoa mafunzo kwa nchi 15 walizozigawanya katika nchi za Afrika na Uarabuni, kujumuisha Misri na Lebanon.

> **"Changamoto kuu wanayokumbana nayo wanawake, ni kutoonekana katika kipindi cha upandishwaji vyeo. Hii inachangia wao wenyewe kutokujiamini na unyanyasaji wa wanawake unaoendelea maofisini.**



Nyingine ni nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, zinazojumuisha Tanzania, Uganda, Kenya, Rwanda, Botswana, Malawi, Somalia, Zambia na Zimbabwe.

Anasema, wanawake wengi wanahitimu elimu ya juu ya uandishi wa habari, lakini wanakumbana na vikwazo katika nafasi za juu za uongozi.

Hivyo Jane anaeleza lengo lililopo ni ama kumpunguzia au kumuondoa kabisa vikwazo, mwanahabari wa kike ili afanikiwe katika kupata vyeo, sehemu za kazi mahali waliko.

"Changamoto kuu wanayokumbana nayo wanawake, ni kutoonekana katika kipindi cha upandishwaji vyeo. Hii inachangia wao wenyewe kutokujiamini na unyanyasaji wa wanawake unaoendelea maofisini" anasema Jane.

Anaongeza :"Hivyo, programu hii inalenga kumjengea uwezo wa kiungozi mwanamke, ili ajiamini na aweze kusimama na kujiuza, pasipo kuhofu uwepo wa mwanaume"

Kingine kinachoambatana na hicho, anakitaja kuwa ni mbinu za kupambana na changamoto katika kuwania nafasi za juu, jambo linalosaidia wasikandamize na kudharauliwa.

Tamala Chirwa, anajivunia kuwa sehemu ya mradi huo kwa miaka minne akiwa Meneja Mradi na Mkufunzi kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati .

"Silaha kuu ya mwanamke katika kupigania haki yake ya kuongoza ni kutokata tamaa, hivyo tunawawafundisha wanawake hawa kuitumia silaha hiyo" anasema Tamala .

### HATUA YA MAFANIKIO

Tangu kuanza kwa mafunzo haya nchini Tanzania mwaka 2015 waandishi wa habari wanawake 24 wamenufaika na baadhi yao kupanda vyeo katika sehemu zao za kazi.

Dk. Joyce Bazira, mkufunzi wa taifa katika mradi huo na mkongwe katika uandishi wa habari, anasema mradi huu ulianza nchini Tanzania mwaka 2015 ikiwa na washiriki watano, idadi yao ikiongezeka kila mwaka hadi washiriki tisa mwaka huu.

Kwa mujibu wa Dk. Bazira, ongezeko la waombaji linatokana na mabadiliko makubwa ya kifikra yanayoonyeshwa na washiriki waliopitia mafunzo katika vyombo vya habari wanakotumikia.

"Washiriki waliopita wamekuwa sumu ya mfumo dume katika vyombo vya habari, wamesimama kidete kushindana na wanaume na hatimaye baadhi yao kupandishwa vyeo" anajivunia Dk. Bazira.

Meneja Jane, anatetea mafunzo wanayotoa kwa wanawake, yameleta mabadiliko makubwa chanya, katika mtazamo wa kiuongozi tofauti na walivyokuwa awali.

"Baada ya mafunzo wanakuwa wanajiamini zaidi, wanakuwa na hamu ya kupiga hatua mbele zaidi ya walipokuwapo na tuna ushuhuda wa baadhi ya wanawake ambao walipanda vyeo baada ya kupata mafuzo haya" anasema Jane .

### USHUHUDA

Beatrice Bandawe, Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, ni shuhuda wa mafanikio yanayopatikana katika mafunzo hayo, pindi mnufaika anapoyazingatia kwa makini.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo mkuu wa gazeti hili, mara baada ya kumaliza programu hiyo ya mafunzo mwaka 2016, aliyarejesha kwa vitendo kazini, hali iliyojionyesha kwa kupandishwa kufikia cheo alicho nacho sasa.

"Naweza kusema cheo hicho kwa kiasi kikubwa. kimetokana na mafunzo ya WIN, maana yalinipa ujasiri wa kuonyesha uwezo wangu wa kiuongozi hadi kuonekana nastahili kuwapo hapa" anaeleza Beatrice.

Beatrice anafafanua kuwa, mbali na kujifunza uongozi, pia kuna ya ziada aliyoyapata ambayo sasa naye anayatumia kufundisha anaowaongoza, akitaja mambo kama vile kujithamini, kujiamini na kuzingatia muda, ambao ukishapita haurudi tena.

Ushauri wake kwa waandishi wanawake ni kwamba, watumie vyema fursa hiyo za bure inayotolewa na Win, kwani ina mengi yenye manufaa kwao.

Mnufaika mwingine naye kutoka Nipashe, ni Salome Kitomari, ambaye ni Mhariri Msaidizi wa Habari, anakiri programu hiyo imembadilisha kwa mengi, kuanzia maisha binafsi hadi kikazi, kwa kuwa amefanyia kazi safari yake kitaaluma na mabadiliko mazuri kazini.

"Katika safari ya kukua kitaaluma ya miaka mitano, nimemaliza chuo kikuu na sasa nina shahada ya kwanza ya mawasiliano ya umma na sasa naendelea mbele,"anasema.

Aidha, Salome ambaye sasa ni mdau mwandamizi katika jumuiya za kutaaluma za uandishi wa habari, kitaifa na kimataifa, anataja mafanikio mengine anayoamini yametokana na kushiriki kozi hiyo.

Anaanza kwa kudokeza kuwa sasa amefikia nafasi ya juu kuwa miongoni mwa wanaofanya uamuzi wa juu gazetini, inayoundwa na vikao, akiwa Mhariri Msaidizi wa Habari.

Katika mtazamo unofanana na wa Beatrice, Salome anasema tangu kupata mafunzo hayo, imani kwa anaofanya nao kazi imeongezeka maradufu, akijivuna amejiongezea maarifa kupitia mafunzo ya muda mfupi ya ndani na nje.

Salome anaendelea:"Kupitia kazi zangu, mwaka jana nilitambulika kuwa mshindi wa jumla wa tuzo za umahiri wa uandishi wa habari Tanzania, ikiwa mara ya kwanza kwa IPP Media(Mashirika ya habari chini ya kampuni ya IPP) kupata tuzo ya juu kwa historia ya miaka 10 ya mashindano hayo yaliyo chini ya Baraza la Habari Tanzania (MCT)."

Mama huyo, anaaamini mafunzo hayo yamemkweza akaaminika kuwa kiongozi kwa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA Tan) anayoiongoza tangu mwaka 2017.

Katika hilo, Salome anataja sehemu ya mafanikio makubwa aliyo nayo ni kuhakikisha mikutano ya kikatiba inafanyika na kutoa utetezi na mafunzo kwa waandishi nchini, ikiwamo kukutana na viongozi kwa ajili ya kushinikiza mabadiliko ya sera na sheria zinazoisimamia taaluma ya habari.

Salome anadokeza sehemu ya mchango wake, ni kuwasaidia wanawake wengine kutumia fursa mbalimbali, bila kujali ugumu uliopo, silaha kuu kwao ni ya dhati katika kutenda jambo.

### CHANGAMOTO JE?

Jane anasema changamoto wanayokumbana nao katika vita hivyo kwa kuwakweza kinamama, ni ukosefu wa pesa za kutosha kwa ajili ya kuendesha mafunzo kwa washiriki wengi zaidi.

"Mwaka huu nchini Tanzania maombi yalikuwa mengi na wengi wao walistahili kupata mafunzo haya, lakini imetulazimu kuchukua (watu )tisa tu kutokana na ufinyu wa bajeti" anasema Jane.

Kasoro nyingine anayoitaja ni uhalisi wa washiriki wanakuwa kazini, hivyo inaweka mtihani katika utekelezaji wake na Mkufunzi wa Taifa Dk. Bazira anafafanua zaidi:

"Unajua kuchukua muda mwingi wa mwandishi haiwezekani, kwa sababu wanakuwa na ratiba zao, mikutano ya kuhudhuria siku za mbele, kwa hiyo hatupati muda wa kutosha wa kuwapa mafunzo."

# Biashara katika picha



Mfanyabiashara wa viazi akihesabu kipato, wakati akisubiri wateja katika soko la Kilombero, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**



Mfanyabiashara ndogondogo Machinga, akisukuma toroli lililosheheni bidhaa mbalimbali akitafuta wateja katika eneo la Chang'ombe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wachuuzi wa machungwa, wakiyapakia kwenye matenga kwa ajili ya kuyatembeza mitaa kwa wateja, baada ya kuyanunua katika soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

BIASHARA

# Ewura walivyopania mwisho wa 'vishoka' umeme Nyanda za Juu




Moja ya kituo cha mafuta jijini Mbeya. **PICHA: MTANDAO.**

**INATOKA UK.13**

Mwanasheria Mkuu wa Ewura, Nzilla Masunga, anasema sheria inaelekeza kwamba, mtu akifanya kazi za umeme bila ya kuwa na leseni kutoka Ewura, adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano au faini isiyozidi milioni 10 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Masunga anasema, yanayolengwa na sheria hiyo ni katika kumpa husika uwezo wa kuunganisha mifumo ya umeme, uzalishaji wake.

Pia, anataka eneo la kusafirisha umeme, usambazaji na ugavi wake, uendeshaji wa mifumo ya umeme, biashara yake na kuvuka mipaka ya nchi kuuziana umeme.

Ni wazi kuwa, hatua hiyo ya kuwatambua mafundi umeme wenye vigezo vya kupatiwa leseni inayofanywa na Ewura, itaisaidia serikali kutimiza ndoto yake kuhakikisha kila Mtanzania anafikiwa na huduma ya umeme, ambayo haitakuwa na madhara kutokana na kuunganishiwa na mafundi umeme wenye vigezo.

Mhandisi Mkuu wa Uzalishaji Umeme wa Ewura, Erick Rugabera, anasema utoaji leseni za uunganishaji mifumo ya umeme kwa watu binafsi, unalenga kutoa utaratibu wa kazi husika kisheria, wenye mwongozo unaoainisha madaraja ya leseni zinazotolewa na mamlaka hiyo, kwa kuzingatia taaluma na uzoefu wa mwombaji.

> **Mafundi wengi wasio na uwezo na elimu sahihi kuhusu vifaa umeme vinavyofaa, hujikuta wanaingia kwenye mtego wa kununua vifaa visivyokidhi viwango na kuishia katika majanga yaliyotajwa kwa jamii.**

Anasema, ni hatua inayo lenga kukabiliana na wimbi la 'vishoka' wanaozurura mitaani na kuwaunganishia watu wenye umeme kinyemela, hivyo kusababisha madhara makubwa katika jamii.

Mhandisi Rugabera, anataja maeneo ya madhara ni nyumba kuungua kwa nyumba au hitilafu za kila mara mahali kulikounganishwa umeme, zinazosababishwa na uunganishaji umeme, bila ya kufuata matakwa ya kitaaluma.

Pia, Nicodemus Mpizi, ni fundi umeme kutoka eneo la Songwe, Mbeya, anamuunga mkono Mhandisi Mkuu wa Ewura, akisema wengi wanaofanya kazi bila ya kusajiliwa na Ewura, matokeo ya kasi zao yamekuwa chini ya kiwango, hali inayochangia ya madhara ndani ya muda mfupi baada majengo kukamilika.

Anasema, mafundi wengi wasio na uwezo na elimu sahihi kuhusu vifaa umeme vinavyofaa, hujikuta wanaingia kwenye mtego wa kununua vifaa visivyokidhi viwango na kuishia katika majanga yaliyotajwa kwa jamii.

Fundi Mpizi anasema, ni wakati muafaka kwa jamii kuhakikisha inashirikiana na mamlaka ya udhibiti kuhakikisha wimbi la vishoka katika jamii linaisha, hivyo kuwezesha mafundi umeme wenye vigezo wafanye kazi kwa ufanisi.

**NYANDA ZA JUU**

Meneja Ewura Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Karim Ally, anaweka wazi ofisi hiyo inafanya jitihada kuhakikisha wenye vigezo na taaluma ndio wanapata leseni za kuunganisha mifumo ya umeme, ili kupunguza madhara na hitilafu za umeme kwenye majengo.

Kwa mujibu wa meneja huyo, madhara yanayojitokeza katika jamii yake, ni uwekaji mifumo duni ya umeme isiyozingatia taaluma, ikiwa ni kazi ya 'vishoka' ndani ya jamii.

Ally anasema, hivi sasa kumekuwapo kasi kubwa ya watu kuunganishiwa huduma ya umeme mijini na vijijini, kutokana na jitihada za serikali kufikishia umeme kwa wengi nchini.

"Unajua kuna miradi mikubwa ya umeme, ukiwemo ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere katika Mto Rufiji na ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 2,115 ambao walengwa wa mradi huo ni Watanzania wote," anasema.

Meneja huyo anasema, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, imejipanga kuhakikisha wananchi wanufaika katika njia sahihi, kwa kuwa na wenye vigezo pekee katika kazi ya uunganishaji umeme huo majumbani, pasipo kusababisha madhara ya kiuchumi, kijamii na kiafya.

Mhandisi Ally anasema miongoni mwa majukumu ya Ewura, ni kutoa leseni na kusimamia utekelezaji wake, kudhibiti ubora, usalama na tija kwa watoa huduma, kutathmini na kupitisha marekebisho ya huduma na kusikiliza malalamiko, pia kutatua migogoro.

Kwa mujibu wa meneja huyo, Ewura inasimama nafasi ya elimu kwa umma kuhusiana na huduma zinazodhibitiwa na mamlaka hiyo.

Mhandisi Ally anasema, Ewura imekuwa ikifanya kazi kwa kuzingatia nyenzo za udhibiti ikiwamo sheria za sekta husika, ikiwamo Sheria za Umeme (2008), Mafuta (2015) na Maji ya mwaka 2019.

Anakumbusha chimbuko la Ewura, ni uwepo wa mamlaka za udhibiti nchini unaotokana na mageuzi ya kiuchumi na sera ya ushindani na udhibiti ya mwaka 1999, inayotambua sekta binafsi katika utoaji mchango kwenye uchumi na kwamba taasisi za umma lazima zijiendeshe kibishara.

Anasema, ni lazima jamii ifahamu kuwa Ewura inadhibiti huduma za nishati (umeme, petroli na gesi asilia), maji na usafi wa mazingira, udhibiti anaojisifu umesaidia kupunguza gharama za udhibiti na kuwezesha mapato ya tozo ya sekta ya nishati, kugharamia sehemu ya gharama za udhibiti za

**INAENDELEA UK.19**

BIASHARA

# Ewura walivyopania mwisho wa 'vishoka' umeme Nyanda za Juu

INATOKA UK.18

sekta za maji.

Meneja Ally anasema, pia Ewura imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi, kuhusu huduma hizo, lengo ni kuharakisha uelewa wa matumizi ya nishati za umeme na gesi majumbani.

"Elimu hii ya uunganishaji wa umeme na matumizi ya gesi kwa watoa huduma na wananchi, ni endelevu katika mikoa yote iliyopo katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ikihusisha mkoa wa Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Njombe na Ruvuma," anasema

Mkaguzi wa Petroli Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jackson Makaya, anaweka wazi kuwa Ewura mekuwa makini katika kuhakikisha inadhibiti matumizi ya gesi ya kupikia kwa wananchi ili kuepusha madhara yasiyo ya lazima katika jamii.

Makaya anasema Ewura inasimamia viwango vya ubora wa bidhaa na miundombinu, kulinda usalama wa wanaotumia gesi ya kupikia majumbani, kupanga bei na kuchochea ushindani kwa watoa huduma za gesi.

Anaendelea kusema kwamba, wanatoa elimu kwa wasambazaji wakubwa na wadogo wa gesi, ili kuhakikisha kunakuwapo matunzo yanayofanywa kwa namna salama, kuepusha majanga yasiyo ya lazima.

Makaya anasema, kumekuwapo kampeni za utoaji elimu ya mazingira sahihi ya kuhifadhi mitungi ya gesi, sambamba na kuhakikisha wote wanaojihusisha na usambazaji wa gesi za kupikia wanakuwa na leseni kisheria.

Anasema, tangu timu ya Ewura iweke mkakati wa utoaji elimu kwa umma ikihimiza matumizi sahihi ya gesi ya kupikia, baada ya kuwapo idadi kubwa ya watumia nishati hiyo nchini, kutokana na gharama nafuu.

Mkaguzi huyo wa Petroli, anakiri kuongezeka uelewa anawasisitiza watumiaji wote wa gesi ya kupikia kuwa mabalozi sahihi katika utoaji elimu hiyo kwa wananchi wengine.

**MKURUGENZI EWURA**

Mkurugenzi mkuu wa Ewura Mchany, katika tarauyfa yake iliyosomwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano na Uhusiano wa mamlaka hiyo,Titus Kaguo, katika mafunzo kwa mafundi umeme mkoani Mbeya, ilianisha majukumu yao muhimu ni kusimamia shughuli za sekta ndogo ya umeme, zinazojumuisha ufungaji wa umeme majumbani.

Anasema uamuzi wa kutoa elimu kwa wadau ni kuwawezesha kufanya shughuli kisheria na kanuni zilizopo.

"Kuna wakati makandarasi huona kama wanaonewa kwa kuhitaji kusajiliwa na kupewa leseni, lakini ikumbukwe kuwa hili linafanyika nchi nzima kwa sababu za usalama na ndiyo maana kila mdau hana budi kutambuliwa na kupewa leseni," anasema Kaguo

Anasema, lengo la kuanzishwa Ewura ni kudhibiti huduma za nishati na maji na kuhakikisha zinatolewa katika viwango stahiki, kinachoendana na gharama sahihi kwa umma, huduma zipatikane muda wote, kwa namna salama na uhakika kwa watumiaji.

Kaguo anasema, umefika wakati Watanzania kuwa na utamaduni wa kuwatumia watalaamu wenye leseni za Ewura, kutandaza nyaya za umeme katika majengo yao, kuepuka hatari na hasara kwao na serikali

Taarifa za Wizara ya Nishati ya Mwaka 2018/19 katika Bunge la Bajeti, zinaainisha Tanzania ilikuwa na ziada ya umeme megawati 300 kwa siku, ikilinganishwa na upungufu wa megawati 100 kwa mwaka 2015.

Pia, hadi kufikia Mei 2019, inaelezwa juhudi za usambazaji umeme imeshavifikia vijiji 7,127 ikilinganishwa na 2018 vilivyokuwa vimeunganishwa mwaka 2015.

Takwimu za wizara hiyo kupitia Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), zinaonyesha kati ya Julai, 2015 hadi Mei, 2019 kuna jumla ya wateja 969,431 waliunganishwa umeme na hiyo ni sawa na wateja 2,442,648 waliokuwepo kufikia Mei, 2019 hapa nchini.



Kushoto ni Meneja wa Ewura Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mhandisi Karim Ally, akitoa elimu kwa wadau kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu nishati ya umeme, petroli, gesi asilia, maji na usafi wa mazingira. **PICHA: INNOCENT NG'OKO**

> **Pia Ewura imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi, kuhusu huduma hizo, lengo ni kuharakisha uelewa wa matumizi ya nishati za umeme na gesi majumbani.**



Mafundi wa Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania (Tanesco) mkoani Rukwa, wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO.**

UCHUMI

MARA YA KWANZA...

# Tuzo za Tehama kwa waimarishaji biashara katika sekta mawasiliano

• Sekta Posta, Simu, Utangazaji



Watu wakipata huduma ya mtandao, kupitia kompyuta mpakato yao. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

**Na Joseph Mwendapole**

HIVI karibuni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), ilianzisha tuzo kwa watoa huduma za mawasiliano wenye leseni za mamlaka hiyo kushiriki tuzo za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Ni mara ya kwanza tuzo hizo kuandaliwa hapa nchini na kwa mujibu wa Mamlaka hiyo, nia ni kuwatambua na kuwatunuku watoaji huduma bora za mawasiliano ili waongeze ubunifu katika utoaji wa huduma za utangazaji.


Lengo lingine la TCRA, ni kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za mawasiliano katika sekta za posta, simu, utangazaji na intaneti na kuongeza chachu na mchango wa sekta ya mawasiliano.

Mamlaka hiyo imeeleza namna gani wahusika watashiriki na kura zitakavyopigwa na washindi watakavyopatikana.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, John Kilaba, mwisho mwa uwasilishaji nia ya kushiriki tuzo hizo ilikuwa Jumapili iliyopita, Machi 15.

TCRA inasema wenye leseni za mamlaka hiyo wote wanatakiwa kuomba kushiriki katika tuzo hizo kwa muda uliowekwa na wananchi watahimizwa kupiga kura ya mtoa huduma anayetoa huduma nzuri zaidi.

> **"Uteuzi wa mwisho utajumuisha mapendekezo ya kura za wananchi pamoja na usaili utakaofanywa na jopo la majaji hatua ambayo itafanyika kuanzia Mei 2 hadi Mei 10 mwaka huu.**



Mahali kunakopatikana huduma ya intaneti kibiashara. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kwenye uzinduzi wa tuzo hizo uliofanyika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Januari mwaka huu na makundi ya washiriki iliwekwa kwenye tovuti maalum ya TCRA ili wadau waweze kujua makundi yanayoshiriki tuzo hizo.

**MKUU TEHAMA**

Mkurugenzi wa Tehama wa TCRA, Connie Francis, anasema kutakuwapo tuzo 17 kwenye shindano hilo, wakiwemo watoa huduma bora wa simu, huduma za intaneti na mtoa huduma bora wa miundombinu ya utangazaji.

Anawataja wengine, ni mtoa maudhui mtandao bora wa blogu, kituo bora cha utangazaji wa televisheni kitaifa, kituo bora cha utangazaji wa televisheni kiwilaya, chaneli bora ya kitaifa inayotazamwa kwa kulipia na mtoa maudhui mtandao bora wa televisheni.

Wengine ni mtoa huduma bora wa kitaifa wenye maudhui yanayotazamwa kwa kulipia kwa njia ya satellite, kituo bora cha utangazaji wa redio cha kitaifa na kituo bora cha utangazaji wa redio cha kimkoa.

Kwa mujibu wa Connie, kundi lingine ni kituo bora cha utangazaji cha redio cha wilaya, kituo bora cha utangazaji wa redio kijamii, mtoa maudhui bora wa redio na mtoa huduma bora wa usafirishaji vifurushi na vipeto wa kimataifa.

Connie anasema mchujo wa awali kwenye tuzo hizo, utafanyika mwezi huu ambao idadi ya mawasilisho yaliyochaguliwa yatachapishwa kwenye tovuti ya mamlaka hiyo.

Aidha, anasema kuanzia mwezi ujao, wananchi watapiga kura kwa njia ya mtandao kwa kupitia tovuti ya TCRA na kwa kutuma ujumbe mfupi kwenye namba ya bure waliyoiweka.

Connie anongeza kuwa uteuzi wa mwisho utajumuisha mapendekezo ya kura za wananchi pamoja na usaili utakaofanywa na jopo la majaji hatua ambayo itafanyika kuanzia Mei 2 hadi Mei 10 mwaka huu.

Anasema mchakato wa kutathmini kila kundi utakuwa wa hatua tatu ambazo ni tathminji ya awali kwa washiriki wote kuzingatia utekelezaji masharti ya leseni ya TCRA, maoni ya wananchi kwa kupiga kura ambapo washiriki walioshiriki mchujo wa awali watapat asilimia 10.

Connie anasema, kwenye tathmini ya kina watakaokidhi vigezo na masharti ya leseni watapata asilimia 30, uvumbuzi, ubunifu na matumizi bora ya Tehama asilimia 20 na ubora na umuhimu wa huduma zitatolewa asilimia 20.

Anasema unafisi wa tuzo hizo unategemea sana wingi wa washiriki kwani TCRA ingependa kuwa na washiriki wengi ili washindi wawe wanabadilika, badala ya kuwa na mshindi mmoja kwa muda mrefu.

Connie anasema, kuwa lengo ni kuimarisha sekta hiyo, basi itapendeza zaidi kama washindi watakuwa wanabadilika mwaka hadi mwaka na kwamba hilo linawezekana tu kama kutakuwa na ushindani mkali.

"Tunataka mwisho wa siku washiriki wote wawe kama washindi yaani mtu anayeongoza aongoze kwa asilimia ndogo sana tunataka tufike hapo kwa hiyo watoa huduma wote wa mawasiliano tunawahamasisha washiriki," anasema Connie.





Mwonekano wa eneo la wazi kwenye mpaka wa Tanzania na Zambia mjini Tunduma, mkoani Songwe jana, baada ya nyumba zilizokuwa zimejengwa na wananchi kubomolewa kwa makubaliano ya serikali za nchi hizo mbili na kuzuia shughuli zingine kufanyika. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Vijana watakiwa kugombea udiwani, ubunge mwaka 2020

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

VIJANA wameshauliwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, kwa maelezo kuwa taifa linawategemea wao kama nguvu kazi ya kuharakisha maendeleo ya nchi.

Kauli hiyo ilitolewa jana na mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Stephen Mwakajumilo, wakati akizungumza na gazeti hili, na kuweka wazi kuwa vijana ndiyo tegemeo kubwa katika ujenzi wa taifa lolote duniani.

Alisema ni wakati mwafaka kwa vijana kujitokeza kuwania nafasi za uongozi ndani ya CCM kwa kuwa chama na taifa vinahitaji maarifa na weledi wao katika kuharakisha mustakabali wa maendeleo ya nchi.

Mwakajumilo alisema vijana wenye sifa wana nafasi kubwa ya kugombea katika nafasi za udiwani na ubunge katika uchaguzi ujao ndani ya chama hicho kutokana na chama kutambua umuhimu wao kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Alisema wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM ni watunga sera na wana wajibu wa kusimamia utekelezwaji wake, na kwamba wabunge ndiyo watekelezaji wa ilani ambayo ndiyo inayoongoza dola kwa sasa.

Alisema kuna changamoto ya baadhi ya wabunge ambao wamekuwa wakishindwa kufika katika majimbo yao kusikiliza kero na changamoto za wananchi na kuziwakilisha serikalini, na kuwa hiyo siyo.

Alisema wajumbe wa Halmashauri Kuu wana wajibu wa kukutana mara kwa mara na wanachama ndani ya mkoa kwa lengo la kukumbushana mambo mbalimbali, yakiwamo kusikiliza na kutoa kero zinazowasibu katika maeneo yao.

Alisema katika kutumikia nafasi hiyo, atahakikisha sehemu kubwa ya ziara zake anafanya katika kata zilizo pembezoni mwa wilaya anayoenda kwa lengo la kukuza upendo, umoja miongoni mwa wanachama ndani ya CCM.

# Ujangili wapungua kwenye hifadhi tatu

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

VITENDO vya ujangili katika hifadhi za taifa za Ruaha, Kitulo na Katavi katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, vimepungua kwa kiasi kikubwa.

Imeelezwa hakuna mizoga ya tembo iliyokutwa ndani ya hifadhi hizo kwa miaka miwili mfululizo, vinavyotokana na viashiria vya ujangili.

Kauli hiyo ilibainishwa jana na Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi Kanda ya Kusini-Tanapa, Dk. Chistopher Timbuka, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusiana na hali ya vitendo vya ujangili katika sekta ya utalii ukanda wa kusini.

Alisema katika hifadhi hizo kuna askari wa kutosha na vifaa vya kisasa kwa ajili ya kukabilina na ujangili, hivyo majangili wengi pamoja na mitandao iliyokuwa inajihusisha na ujangili imepotea kutokana na baadhi ya majangili hao kukamatwa na kuchukuliwa hatua.

Alisema serikali imeweka nguvu kubwa katika kukabiliana na vitendo vya ujangili katika hifadhi, kuwa na hali ya ujangili imepungua sana na wanyama kama tembo, nyati na twiga wanazidi kuzaliana kwa kasi kutokana na kuishi kwa amani.

Aidha, alisema kumekuwa na udhibiti mkubwa wa ujangili unaotokana na uvunaji wa zao la chikanda katika Hifadhi ya Taifa ya Kitulo kutokana na zao hilo miaka ya nyuma kuwa na soko kubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi na nchi jirani za kusini mwa Tanzania.

Alisema zamani kulikuwa na mtandao wa majangili wa zao hilo uliokuwa unajumuisha wafanyabiashara waliokuwa wanasafirisha zao hilo katika maeneo tofauti ya nchi na nchi jirani za kusini mwa Tanzania, lakini hadi sasa hali ni salama kabisa kutokana na askari kufanya doria muda wote ndani ya hifadhi na ushirikiano mzuri na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo.

Alisema mbali na uwapo wa askari waliopewa mafunzo ya kutosha na vifaa vya kisasa vya kukabiliana na ujangili, kumekuwa na ushirikiano mzuri na wananchi wanaoishi karibu na hifadhi, na wamekuwa ni msaada mkubwa katika mapambano ya kuwatokomeza majangili hao.

Kwa mujibu wa Timbuka, ujangili wa wanyama kama tembo umebaki historia katika hifadhi za taifa za Ruaha na Katavi katika ukanda wa kusini kwa kuwa kuna doria na msako mkali wa njia mbalimbali ukiwepo msako wa kutumia ndege na askari wanaotumia magari.

Ili kuimarisha ujirani mwema, Dk. Timbuka alisema kuna timu ya watu mbalimbali ambayo ipo katika Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya inatoa elimu kuhusiana na mambo mbalimbali ya ujirani mwema na mapambano shirikishi miongoni mwa wananchi na serikali dhidi ya ujangili na manufaa ya hifadhi za taifa katika maeneo yao.

# Kada CCM achangia nyumba ya mchungaji

**Na Innocent Ng'oko,** MBEYA

MJUMBE wa Kamati ya Siasa wa Chama Cha Mapinduzi(CCM) Mkoa wa Mbeya, Gulzar Sabir, amechangia mifumo 10 ya saruji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kirutheri Tanzania (KKKT) Mtaa wa Tazara Usharika wa Rujewa wilayani Mbarali ili kumwezesha kuwa na makazi ya kudumu.

Akikabidhi msaada huo jana, Gulzar alisema jamii inawajibu wa kujenga utamaduni wa kujitoa kwa ajili ya kusaidia uhitaji katika nyumba za ibada kwa lengo kujenga umoja na mashirikiano miongoni mwa jamii nchini.

Alisema uamuzi wa kutoa msaada huo wa mifuko kumi ya saruji katika KKKT ni kutokana na kuguswa na malengo ya kanisa hilo ya kuwajengea viongozi wa dini nyumba za kuishi baada ya kustaafu huduma za Mungu katika jamii.

Gulzar alisema kuna wakati ni lazima kila mwananchi aone umhimu wa kujitolea katika nyumba za ibada kutokana na kuwa viongozi wa dini na waumini wao wamekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi, ikiwamo ya kuwaombea viongozi wa kitaifa na taifa dhidi ya mambo mabaya ambayo yanaweza kujitokeza.

Katibu wa KKKT mtaa wa Tazara Ushirika wa Rujewa, Peter Nsemwa, alisema kumekuwa na changamoto ya wainjilisti wengi wa kanisa hilo baada ya kustaafu wanakosa makazi ya kudumu kwa ajili ya familia zao na wengi wao wamekuwa wakiishia maisha magumu.

"Tumelazimika kuanzisha utaratibu wa kanisa wa kuwajengea nyumba binafsi watumishi ili wanapostaafu wawe na makazi rasmi ya kuishi badala ya kutangatanga kutokana na kukosa makazi licha ya kumtumikia Mungu kwa muda mrefu," alisema Nsemwa.





# Madaktari wazawa sasa wapandikiza figo Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa (BMH), kwa mara ya kwanza imepandikiza figo kwa mgonjwa, Emanuel Kahigi, kutoka mkoani Geita ikitumia madaktari wazawa bila kutegemea wataalamu kutoka nje ya nchi.

Awali, upandikizaji wa figo ulikuwa ukifanywa hospitalini hapo kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) na wataalamu kutoka Tokushukay Medical Corporation ya Japan.

Akizungumza na waandishi wa habari hospitalini hapo jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika, alisema madaktari hao wamefanya upasuaji huo kutokana na kupata ujuzi kutoka kwa wataalamu hao wa Japan.

Alisema kwa kiasi kikubwa wametimiza walichokiahidi kwa Watanzania, akibainisha kuwa walifanya upandikizaji huo Machi 3 mwaka huu na mgonjwa huyo anaendelea vizuri.

Dk. Chandika alisema kupitia wataalamu hao kutoka taasisi mbili za Japan, imesaidia kwa kiwango kikubwa kutoa utaalamu na kuchangia gharama za kuishi kwa wataalamu wa hospitali hiyo waliokwenda katika nchi hiyo kujifunza upandikizaji figo.

"Tutaendelea kushirikiana nao kama kutakuwa na mgonjwa atakayekuwa na shida kubwa zaidi kwenye upandikizaji. Tunafurahi kwa mara ya kwanza tangu Tanzania iundwe, tumepandikiza figo bila kutumia wataalamu kutoka nje na huduma hii inapatikana kwa gharama nafuu," alisifu.

Alisema wataangalia namna ya kuanzisha kozi maalum za kujifunza upandikizaji ili kusaidia wataalamu wengine wa ndani na wa nchi jirani.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Udom aliyeshiriki upandikizaji huo, Dk. Masumbuko Mashambwa, alisema upandikizaji huo ulichukua saa 10.

"Tulichukua saa 10 kutokana na kwanza ndiyo mara ya kwanza kufanya wenyewe na kulikuwa na shida ndogo ndogo, sasa tunapandikiza figo bila shida yoyote, na wagonjwa watakaopata wagonjwa wenye shida hiyo tunawakaribisha kuja Benjamin Mkapa," alisema.

Daktari huyo alisema uhitaji wa upandikizaji figo ni mkubwa nchini. "Madaktari hasa wanaohudumia wagonjwa wenye matatizo ya figo wanaotumia mshipa mkuu wa damu (Femoral Vein) wasitumie mshipa huo wa kulia kwa kuwa inasababisha kuleta shida wakati wa upandikizaji," alishauri.

Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Figo, Dk. Kessy Shija, alisema kulikuwa na wagonjwa wengi waliokuwa wanapelekwa nje ya nchi kwa ajili ya huduma hiyo, lakini serikali imeendelea kuimarisha huduma za kibingwa ili wagonjwa watibiwe nchini.

"Hizi huduma tutafanya mara kwa mara, tunaomba wananchi waje kwa sababu sasa upandikizaji figo unapatikana nchini na tatizo limekuwa kwa wale wanaotoa figo kwa ndugu, naomba niwaambie hakuna tatizo lolote ukitoa huduma kiungo chako kimoja kumsaidia ndugu yako," alisema.

Alisema mgonjwa aliyepandizwa figo, aliugua kwa muda mrefu na hakuwahi kuona mkojo wake kwa miaka mitano, lakini sasa amepata.

"Ilikuwa ni ndoto kwake, chukulia miaka mitano bila ya kupata mkojo, halafu unakuja kupata kwa kweli ilikuwa furaha kwake," alisema.



Diwani wa Kata ya Majengo, jijini Dodoma, Nsinta Mayaoyao (katikati), akikabidhi ndoo za kuwekea maji na dawa kwa mmoja wa mabalozi wa soko kuu la Majengo jana, kwa ajili ya kunawia watu watakaoingia na kutoka wakiwamo wafanyabiashara wa sokoni hapo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Costech yawafunda wabunifu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Sayansi na Teknolojia (Costech), imewataka wabunifu kubuni vitu vinavyotumiwa na watu wengi ili kuchangia Pato la Taifa kupitia soko la ubunifu.

Mratibu wa Habari na Mawasiliano wa taasisi hiyo, Deusdedit Leonard, alitoa rai hiyo jijini hapa jana katika Maonyesho ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ya (Makisatu). Alisema kwa kiasi kikubwa wabunifu wanatakiwa kubuni vitu vyenye tija kwa taifa ili kuchangia Pato la Taifa. "Costech safari hii tumekuja kivingine katika maonesho haya na wabunifu tayari wako sokoni na bidhaa zao zinauzika," alisema.

Alisema mwaka huu taasisi hiyo imepeleka wabunifu wa zabibu, alizeti na nguo katika kongamano la tatu la wabunifu.

"Mwaka jana, Costech ilileta wabunifu lukuki katika mashindano ya Makisatu na walishinda, lakini safari hii tumeamua kuleta wabunifu ambao wamefanikiwa kupitia taasisi hii," alisema.

Aliongeza kuwa taasisi hiyo imefanikiwa kukusanya wabunifu katika kongamano hilo kutoka mikoa mbalimbali nchini na wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wabunifu hao.

# Milioni 200/- kutengwa kutunisha mfuko viziwi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kutenga Sh. milioni 200 katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya mfuko wa viziwi ili kusaidia kutatua kero zinazolikabili kundi hilo.

Kaimu Mkurugenzi wa Kitengo cha Watu Wenye Ulemavu kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Philibert Kawemama, aliyasema hayo mjini hapa alipofungua warsha ya utoaji elimu kwa watu wenye ulemavu wa kusikia kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya.

Kawemama alibainisha kuwa kwa mwaka huu wa fedha, serikali ilitenga Sh. milioni 100, lakini mwaka ujao wanatarajia kuongeza kufikia Sh. milioni 200 ambazo wanaamini zitatatua kero mbalimbali zikiwamo zinazozikabili shule sita za kundi hilo zilizopo nchini.

"Tunajitahidi kuhakikisha tunatokomeza vikwazo vilivyopo ndiyo maana kitengo hicho kimetengewa kiasi hicho cha fedha," alisema.

Kiongozi huyo alisema lengo ni kuona matatizo yanayowakabili yanaisha na kuhimiza kuwa na bima ya afya kama ilivyo kwa watu wengine.

Ofisa wa Bima, Priscilla Lyimo, alisema wametoa elimu kwa kundi hilo ili lijue umuhimu wa kuwa na bima ya afya katika familia zao, akibainisha kuwa ni mara ya nne kutoa elimu kwao na mwitikio ni mkubwa.

"Tutaendelea kutoa elimu kwa watu katika makundi yote, lengo ni kuona kila mmoja anajua umuhimu wa bima ya afya," alisema.

Katibu Mtendaji kwa Taasisi ya Maendeleo kwa Viziwi Tanzania, Kelvin Nyema, aliishukuru serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya watu wenye ulemavu huo.

Alisema anaamini fedha hizo zitasaidia kutatua kero zinazowakabili na elimu waliyopewa itasaidia kujua umuhimu wa bima ya afya.

"Kwa kuwa mwitikio ni mkubwa na serikali imeliona hili, ni vyema kuendelea kuhimiza elimu itolewe kwa jamii ili kuwafundisha umuhimu wa bima ya afya kwa sababu ni kinga," alisisitiza.



## Wakoshwa uboreshaji wa huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu,** UNGUJA

WAGONJWA wenye maradhi yasioambukiza, wameipongeza serikali kwa kuimarisha huduma za afya, hasa dawa za wagonjwa wa kisukari na shinikizo la damu.

Wakizungumza katika mkutano wa uhamasishaji wa vyombo vya habari kuelimisha jamii kujikinga na maradhi hayo ulioandaliwa na muungano wa jumuiya ya maradhi yasioambukiza Zanzibar, wadau hao walisema serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Mohamed Shein, imehakikisha dawa za magonjwa hayo zinapatikana bila ya malipo. Walisema ni ukweli usiopingika kuwa matibabu ya mgonjwa mwenye maradhi hayo ni ghali, hivyo walikuwa wakishindwa kumudu gharama hizo.

"Tunaipongeza serikali yetu, imetusaidia sana wananchi hasa wenye kipato cha chini kwani tungeshindwa kupata matibabu," alisema Mwanamwema Mwalimu, mgonjwa wa saratani.

Alisema baada ya kugundulika kwa tatizo hilo, serikali kupitia Wizara ya Afya ilimsaidia kumpatia matibabu ya awali na sasa hali yake kiafya ni nzuri.

Naye, Faida Omar anayesumbuliwa na shinikizo la damu, alisema kuna kila sababu ya Wazanzibar kumpongeza Rais Shein kwa hatua anazozichukua katika kuimarisha sekta ya afya.

Aliwaomba wananchi kuendelea kuiunga mkono serikali na kujenga utamaduni wa kupima afya zao mara kwa mara ili kujua afya zao mapema.

"Hatuoni sababu ya kuogopa kupima afya zetu mara kwa mara kwani huduma zote zinatolewa bila ya malipo katika hospitali na vituo vyetu vya afya vya serikali," alisema.

Akitoa elimu ya maradhi ya kisukari, Daktari wa Kliniki ya Wagonjwa wa Kisukari Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, Dk. Faiza Kassim Suleiman, alisema vichocheo vya ugonjwa huo ni kutofanya mazoezi, kula vyakula vyenye mafuta mengi na kuwa na unene kupitiliza.

Alisema maradhi ya kisukari ni maradhi ya kudumu na hayatibiki tena, hivyo aliwasisitiza wagonjwa hasa wenye kisukari wenye vidonda kufikia hospitali mapema kupatiwa huduma ya kwanza ili kuepusha kukatwa viungo.

Dk. Faiza alisema wanabahari ni watu muhimu na wana nafasi kubwa ya kuelimisha jamii kujikinga na mambo hatari yanayochochea kupata maradhi.

Katibu wa Muungano wa Jumuiya ya Maradhi Yasioambukiza Zanzibar, Henry Lious Majaaliwa, alisema maradhi ya kisukari yanaongoza kwa kuua watu wengi Zanzibar, hivyo akawataka wanahabari kushirikiana katika kuelimisha jamii juu ya kujikinga na viashiria vya maradhi hayo nchini.

# Corona yazidi kupaisha bei bidhaa

**Na Rahma Suleiman,** UNGUJA

LICHA ya serikali kuwataka wafanyabiashara kutopandisha bei za vifaa visaidizi vya kujikinga na corona, sabuni za kuoshea mikono na maski zimezidi kupanda bei.

Sabuni ya kuoshea mikono, nusu lita ambayo awali ilikuwa ikiuzwa Sh. 12,000, jana iliuzwa Sh. 20,000. "Siku tatu zilizopita, nilinunua dawa ya kuosha mikono ya nusu lita Sh. 12,000, leo hii (jana) nimenunua Sh. 20,000, hii ni hatari sana," alisema Mussa Mbarouk aliyefika kununua dawa hiyo katika duka moja la dawa lililoko Darajani mjini Unguja. Alidai duka hilo ndiyo pekee lenye vifaa hivyo na maduka mengine katika eneo hilo vimeisha, hivyo akaiomba serikali kusimamia suala hilo ili kuwawezesha wananchi kujikinga na virusi hivyo. Juzi, Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhamed, alisema serikali inalaani vikali vitendo vya wafanyabiashara kutumia ugonjwa huo kwa faida zao binafsi kwa kupandisha bei ya vifaa vya kinga, bidhaa na huduma nyingine na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya watakaobainika. Kutokana na kuingia kwa ugonjwa huo visiwani Zanzibar, aliwataka wananchi kuepukana na mikusanyiko isiyo ya lazima. Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Dk. Ali Salum Ali, alisema ni vyema kwa wagonjwa kutumia hospitali zilizoko karibu na maeneo yao ili kuepusha idadi ya watu wengi katika hospitali hiyo.

Alisema hospitali hiyo ni ya rufani, hivyo wanaolazimika kufuata huduma ni wale wagonjwa wenye matatizo maalum.

Mkurugenzi huyo alisema kwa siku hospitali hiyo inapokea wagonjwa 5,000, lakini wengine si lazima wafike hapo kwa kuwa matatizo waliyo nayo yanaweza kushughulikiwa na vituo vya afya vilivyo karibu na maeneo yao na hawana sababu za kufika hospitalini hapo. Alisema hadi sasa, hospitali hiyo bado haijapokea mgonjwa mwenye virusi vya corona.

Ofisi ya Mufti nayo imepiga marufuku mikusanyiko ya watu isiyokuwa ya lazima ikiwamo ya hitima, matanga na kuagiza kuwa katika msiba, jeneza lichukuliwe na watu maalum.

Katibu wa Mufti Zanzibar, Khalid Ali Mfaume, alisema ofisi hiyo pia inawataka waumini kuweka usafi katika nyumba za ibada ikiwamo misikiti kwa kuweka dawa za kuosha mikono ili kujikinga na ugonjwa huo.




Kijana aliyetuhumiwa kuiba simu katika duka moja lililopo eneo la Darajani mjini Unguja juzi, akiwa amelala chini baada ya wananchi wenye hasira kumpiga na kuokolewa na askari polisi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Doria zaongeza mapato ya wavuvi

**Na Rahma Suleiman**
UNGUJA

DORIA katika ukanda maeneo ya Hifadhi ya Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja (Tumca), zimesaidia kudhibiti uvuvi haramu na kuleta matumaini makubwa kwa wavuvi kupata mapato zaidi.

Mkuu wa Doria kutoka Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Haji Shomari, aliyasema hayo baada ya doria iliyofanyika katika ukanda huo.

Alisema doria zimerudisha matumaini ya wavuvi kupata kipato kikubwa kufuatia kuwapo kwa hazina ya samaki baada ya eneo la ukanda huo kuingizwa katika orodha mpya ya hifadhi mwaka jana.

"Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kupitia mradi wa Swiofish kwa kiasi kikubwa imesaidia kupambana na uvuvi haramu na kulinda mazingira ya baharini ikiwamo matumbawe na hivyo kuongeza kiwango cha samaki," alisema. Baadhi ya wavuvi wa ukanda wa ghuba ya hifadhi hiyo, walieleza kufurahishwa na doria hizo ambazo lengo lake ni kuzuia uvuvi haramu na kulinda rasilimali za baharini.

"Sisi wavuvi wa maeneo ya Hifadhi ya Ghuba ya Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja tumefurahishwa na doria zinazofanyika chini ya Idara ya Uvuvi ambazo lengo lake kulinda rasilimali za baharini," alisifu Ali Juma, mvuvi katika eneo hilo.

"Ufugaji na ufunguaji wa uvuvi wa pweza kwa kiasi kikubwa umetuletea neema wananchi wa Kisiwa cha Tumbatu kilichopo chini ya Hifadhi ya Tumca, tunatarajia kupata mavuno mazuri ya pweza," alisema Himid Jongo, mvuvi mwingine katika eneo hilo.

Mradi wa Swiofish unatekelezwa chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ukiwa na lengo la kulinda rasilimali za baharini na kuwawezesha wavuvi wadogo kupiga hatua kimaendeleo.

Mradi huo unahusisha uvuvi uliopewa kipaumbele wa pweza pamoja na dagaa ili kuongeza kipato na kuanzisha kamati za uvuvi kwa lengo la kulinda mazingira.

## Wanahabari wanawake washauriwa kuyafichua yaliyojificha

Na Halima Ikunji, TABORA

WAANDISHI wa habari wanawake mkoani Tabora wametakiwa kufanyakazi zao kwa kuibua mambo yaliojificha ili kuisaidia serikali iweze kuyafanyia kazi.

Rai hiyo ilitolewa na mwezeshaji kutoka Arusha, Sophia Ngalapi wa chama cha wafanyakazi cha JOWUTA Tanzania, kwenye mafunzo ya jinsia na usalama, yalioandaliwa kwa ufadhili wa Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari nchini Norway kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Habari (IFJ).

Ngalapi alisema lengo la mafunzo hayo kwa waandishi wa habari wanawake ni kuona jinsia inatendewa haki wanapokwenda kutafuta habari kwa wadau au ofisi za serikali.

Alisema kwamba waandishi wa habari wanawake nchini wapo wengi, lakini waliopo kwenye nafasi za uongozi katika taaluma yao ni wachache, hivyo aliwataka waongeze bidii kazini na wajiendeleze kusoma na kupitia machapisho mbalimbali ili wapate uelewa mzuri.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa JOWUTA Tanzania, Saidi Mmanga, aliwataka waandishi wa habari wanawake mkoani hapa kwamba ni lazima wawe waangalifu katika kuandika habari wanapokwenda kuzitafuta sehemu mbalimbali katika maeneo waliopo.

Mmanga alisema kwamba mafunzo waliyopata ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari wanawake na jinsi ya kufanyakazi ili kuelimisha jamii.

Kwa upande wao waandishi wa habari wanawake mkoani Tabora wakiwakilishwa na Salma Abdul wa Redio ya Uyui FM, walishukuru kupata mafunzo hayo kwa ufadhili wa Norway.

Alimweleza mwezeshaji huyo kwamba katika tasnia yao kuna changamoto nyingi ikiwamo kutopewa ushirikiano kutoka kwa wadau, kutoaminiwa katika utendaji kazi.

# Wadau wachangia shule tani 5 chakula

Na Sabato Kasika

KATIKA kukabiliana na changamoto za utoro shuleni, wadau mbalimbali wa elimu wamechanga jumla ya tani 5.6 za mahindi na maharage, kwa ajili ya chakula cha wanafunzi wa shule za msingi Sokoine na Chirorwe, zilizopo Halmashauri ya Musoma mkoani Mara.

Tani hizo zilichangwa na wadau hao wakiwamo wazazi, na Shirika la Kimataifa linalojishughulisha na uboreshaji wa afya na kukomesha njaa, kupambana na ugumu wa maisha na kuendeleza wanawake na wasichana la Project Concern International (PCI-WE).

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Musoma, John Kayombo, aliliambia gazeti hili kuwa tani hizo zitatosha kwa muda wa mwaka mmoja na pia mikakati ya kuchangia chakula katika shule nyingine inaendelea.

"Kwa ushirikiano wa shirika hilo na wadau wengine tumechangisha tani hizo za mahindi na maharage, huku Mbunge wa Jimbo Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo akichangia magunia 11 ya mahindi na mengine mawili ya maharage," alisema Kayombo.

Kayombo alisema, huo ni mwanzo wa utekelezaji wa maazimio ya uboreshaji wa elimu katika shule za msingi na sekondari mkoani Mara yaliyofikiwa hivi karibuni, kwenye mkutano wa wadau wa elimu.

Mkurugenzi huyo alitaja moja ya maazimio hayo kuwa ni utoaji wa chakula kwa wanafunzi wawapo shuleni, katika shule zote za msingi na sekondari mkoani humo kama njia ya kuongeza ufaulu.

Aidha, alisema Shirika la PCI-WE lina mchango mkubwa wa kuisaidia kuinua maendeleo ya wanawake wa halmashauri ya Musoma, na kwamba sasa linahudumia vikundi 169 kutoka kata 14 katika halmashauri hiyo.

"Kata hizo ni Bukumi, Makojo, Bugwema, Bukima, Bwasi, Bulinga, Kiriba, Ifulifu, Etaro, Mugango, Nyakatende, Nyegina, Rusoli na Suguti, ambapo pia shirika limetoa baiskeli kwa wakufunzi wa vikundi," alisema.



Baadhi ya wakufunzi wa vikundi vilivyo chini ya Shirika la Kimataifa la kuwezesha wanawake na wasichana la Project Concern International (PCI-WE), katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, mkoani Mara, wakiwa na baiskeli zilizokabidhiwa juzi na shirika hilo, kwa ajili ya kuwarahisishia kazi zao. Kulia ni Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo ambaye alikuwa mgeni rasmi katika makabidhiano hayo. PICHA: MPIGA PICHA WETU

# Bunge laridhishwa mazingira maendeleo mradi reli ya kisasa

Na Mwandishi Wetu

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Viwanda, Biashara na Mazingira imeridhishwa na maendeleo ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na kuwataka wasimamizi wa mradi huo kuendelea kutunza mazingira kama kanuni na sheria za mazingira inavyotaka ili kusiwe na athari za kimazingira baada ya mradi kumalizika.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Suleiman Saddiq, aliyasema hayo walipotembelea mradi huo eneo la Pugu kujionea jinsi unavyoendelea na namna sheria zinavyofuatwa katika usimamizi na uhifadhi na mazingira kipindi chote cha utekelezaji cha mradi.

"Mradi huu ni mkubwa kwa nchi hivyo ni muhimu kuhakikisha kunakuwa na ufuatiliaji wa karibu wa maendeleo ya mradi sambamba na utunzaji wa mazingira," alisema Saddiq.

Alisema Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lishirikiane kikamilifu na wadau wengine katika mradi wa SGR kuhakikisha mazingira yanalindwa ili mradi utakapokamilika athari za kimazingira zisiwapo na kuufanya mradi uishi kwa muda mrefu.

"Elimu kwa wananchi wanaoishi kando ya mradi iendelee kutolewa ili waelewe faida za mradi na pia athari zinaweza kutokana na mwingiliano wa watu jambo ambalo litawasaidia kujilinda na pia kufaidika kupitia fursa zitokanazo na mradi," alisema Saddiq.

Alisema miradi kama hii ishirikishe jamii ili iweze kufaidika kupitia fursa za mradi huo na sehemu ya fedha ya mradi iweze kufanya maendeleo katika maeneo ambayo mradi huo unapita na kuwafanya wananchi waweze kupiga hatua kimaendeleo. "Serikali imetoa kiasi kikubwa cha fedha kufanikisha mradi huu, hivyo ili kwenda sambamba na thamani ya fedha ni muhimu kuhakikisha maendeleo ya mradi yanakwenda sawa na utunzaji na uhifadhi wa mazingira," alisema.

Saddiq alipongeza hatua zinazochukuliwa na Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) kwa kuhakikisha miundombinu ya nishati inaboreshwa na pia upatikanaji wa umeme unakuwa wa uhakika jambo linalotoa uhakika kuwa mradi wa SGR hautakwamishwa kwa sababu ya nishati.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema amepokea mapendekezo na maagizo ya kamati na kuahidi watayafanyia kazi ili kuhakikisha mazingira yanalindwa ili kuufanya mradi kuwa endelevu kwa kizazi cha sasa na baadaye. Naye Mkurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alishukuru kamati hiyo kutembelea na kujionea mradi unavyoendelea na pia alisema mapendekezo yaliyotolewa na kamati watayazingatia ili kuboresha utendaji kazi na miundombinu iweze kuwenda sambamba na uhifadhi wa mazingira.

**HABARI KIMATAIFA**

# Benki Kuu Ulaya yatangaza dharura kusaidia uchumi

**LONDON,** Uingereza

BENKI Kuu ya Ulaya (ECB), imetangaza mpango wa dharura wa ununuzi wa dhamana wenye thamani ya mabilioni ya euro, kwa lengo la kusaidia uchumi wa Ulaya unaoonekana kuathirika na mlipuko wa virusi vya corona.

Janga la mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona tayari limeziweka biashara nyingi chini ya shinikizo, huku baadhi ya serikali zikiahidi hatua za kiuchumi kukabiliana na ukosefu wa ajira.

Katika taarifa yake ECB imesema, mpango huo wa dharura wa ununuzi wa dhamana una thamani ya euro bilioni 750, na utahusisha sekta ya umma na binafsi.

Benki hiyo pia imelegeza baadhi ya vigezo vilivyopo ambako dhamana zinaweza kununuliwa na Benki Kuu.

Mpango huo pia unairuhusu ECB kununua deni la serikali ya Ugiriki. Aidha taarifa ya ECB imeongeza kuwa inaweza kupanua wigo wa mpango huo na vilevile vigezo kwa ajili ya ununuzi wa dhamana kwa kadri inavyohitajika.

Ununuzi huo wa dhamana utafanywa hadi mwishoni mwa mwaka huu na unalenga kuzisaidia sekta zote za uchumi, zikiwamo familia, biashara, benki na serikali.

Ugonjwa wa virusi vya corona ulianza mwaka jana nchini China na kupewa jina la COVID-19 na kuanza kuenea katika mataifa mengi duniani na kusababisha vifo vya wananchi wengi huku wengine wakihifadhiwa katika karantini.

Hadi sasa nchi nyingi za Ulaya zimekuwa zikiathirika na ugonjwa wa virusi vya corona hali inayosababisha biashara kufungwa na watu wengi kujifungua nyumbani.

Mbali na hilo, nchi nyingi za Ulaya zimefunga mipaka yake ambapo hakuna ndege yoyote inayoruhusiwa kuingia wala kutoka katika nchi zao kwa kuhofia maambukizi ya ugonjwa wa virusi vya corona kuenea zaidi. **DW**



# Watalii 1,700 wawekwa karantini hofu ya corona

**CAPE TOWN,** Afrika Kusini

ZAIDI ya watu 1,700 wamekwama kwenye meli ya kitalii na meli ya kubeba mizigo kwenye pwani ya Cape Town nchini Afrika Kusini kwa hofu kwamba baadhi yao wameambukizwa virusi vya ugonjwa wa corona.

Wasiwasi uliibuka kwa mamlaka za bandari baada ya mfanyakazi wa meli ya mizigo, ambaye alikuwa safarini kutoka Uturuki mnamo 9 Machi, alipoanza kuonesha dalili za virusi hivyo.

**Afrika Kusini imethibitisha kuwa na watu 116 walioambukizwa, wengi wao watu waliohusishwa na safari za Ulaya.**

Baada ya kubainika, mfanyakazi huyo alitengwa kwenye meli sambamba na mfanyakazi mwenzake ambaye alikuwa naye kwenye ndege na kutoka Uturuki. Ufuatiliaji wa mawasiliano umebaini kuwa watu wengine sita waliokuwa kwenye ndege hiyo baadaye walienda kwenye meli ya kifahari ya Aidamira.

Hata hivyo, meli hiyo ilianza safari siku iliyofuata, ikitembelea Lüderitz na Walvis Bay huko Namibia kabla ya kurudi Cape Town hivi karibuni. Vyombo hivyo vya majini hubeba raia wa Ujerumani na Australia.

Mamlaka za afya sasa zinasubiri majibu ya watu saba waliokaribiana na mfanyakazi wa meli ya MV Corona aliyekuwa mgonjwa. Wote wamepiwa. Msemaji wa Wizara ya Afya, Popo Maja alisema: "Suala la upimaji ni la lazima".

Afrika Kusini imethibitisha kuwa na watu 116 walioambukizwa, wengi wao watu waliohusishwa na safari za Ulaya.

Hata hivyo, nchi hiyo imeanza kurekodi maambukizi miongoni mwa raia wa Afrika Kusini. **BBC**



Maofisa wa afya nchini Korea Kusini wanaendelea na mapambano dhidi ya kuenea kwa virusi vya ugonjwa wa corona katika mji wa Seoul. **PICHA: AFP**

# Walioambukizwa corona Congo wafikia 14

**KINSHASA,** Congo

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imetangaza visa 14 vya maambukizi ya virusi vya corona nchini humo.

Rais wa DRC, Félix Tshisekedi alitangaza hatua za kukabiliana na kuenea kwa virusi vya ugonjwa huo, ambao Shirika la Afya Duniani, (WHO), liliuita kuwa ni janga la kimataifa.

Daktari Jean-Jacques Muyembe, mratibu wa mapambano dhidi ya virusi vya ebola, sasa ni mratibu wa mapambano dhidi ya virusi vinavyosababisha ugonjwa huo.

"Tuko mwanzoni mwa janga hili. Ugonjwa huu ni tishio kubwa ambalo linataka hatua kali," alisema Rais Tshisekedi.

Hatua zilizochukuliwa na Rais Tshisekedi ndizo zilizotangazwa, zinafanana na zile ambazo tayari zimeanza kutumika katika nchi nyingi duniani.

Hatua hizo ni pamoja na mikusanyiko yote, mikutano, sherehe za watu zaidi ya 20 kwenye maeneo ya umma ni marufuku nchini kote DRC pamoja na shule, vyuo vikuu kufungwa kwa muda wa mwezi mmoja.

Sherehe zote za ibada ya watu wengi na michezo katika viwanja mbalimbali na sehemu zingine za mikusanyiko pia zimepigwa marufuku, Sherehe zote za starehe, baa, migahawa vimefungwa.

Aina zingine za mikusanyiko, kama misiba imewekwa chini ya kanuni maalumu ambapo watu hawaruhusiwi kukusanyika nyumbani kwa marehemu au sehemu yoyote ile.

Utaratibu uliowekwa na serikali ya Rais Tshisekedi ni kwamba mwili unachukuliwa moja kwa moja kutoka chumba cha kuhifadhi maiti kwenda mahali pa mazishi kwa idadi ndogo ya watu wanaosindikiza jeneza.

Rais Tshisekedi pia alichukua uamuzi wa kusitisha safari zote za ndege kutoka nchi zilizoathirika na ugonjwa wa virusi vya corona. **RFI**

# UN: Watu milioni 24 kupoteza kazi kisa corona

**WASHINGTON,** Marekani

UMOJA wa Mataifa (UN) umesema zaidi ya watu milioni 24 duniani wanaweza kupoteza ajira kutokana na athari za ugonjwa wa virusi vya corona.

Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na kazi ILO, limesema ukosefu wa ajira duniani unaweza kuongezeka kufikia watu millioni 5.3 katika kiwango cha chini na watu milioni 24.3 katika kiwango cha juu.

Janga la mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona tayari limeziweka biashara nyingi chini ya shinikizo, huku baadhi ya serikali zikiahidi hatua za kiuchumi kukabiliana na ukosefu wa ajira.

Mkurugenzi wa ILO, Guy Rider, alisema janga hilo siyo tu limekuwa mgogoro wa kiafya duniani, lakini ni janga kubwa katika soko la ajira na mgogoro wa kiuchumi ambao umekuwa na athari kubwa kwa watu. Kati ya watu milioni 8.8 na milioni 35 wanaweza kuwa katika umaskini wa kufanya kazi ifikapo mwishoni mwa mwaka huu kutokana na athari za ugonjwa wa virusi vya corona. **DW**

# Wateja wa Airtel Money wapata gawio bil. 2.6/-

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu za mkononi ya Airtel, jana ilitangaza kugawa faida ya Sh. bilioni 2.6 kwa wateja na mawakala wake wote wanaotumia huduma ya Airtel Money kwa kipindi cha Aprili hadi Septemba, mwaka jana.

Faida itokanayo na Airtel Money ni fedha ambayo kampuni imekuwa ikizirudisha kwa wateja wake waliotumia huduma hiyo kwa kila robo ya mwaka kulingana na kiwango ambacho kimo kwenye akaunti kila siku.

Kiwango hicho cha faida kwa kila salio la mteja kinatolewa pia kulingana na mteja anavyotumia huduma ya Airtel Money na mteja atatumiwa faida yake kwenye akaunti yake na anaweza kuamua kuzitoa, kutuma au kuzitumia kwa matumizi yoyote ikiwamo kulipia bili mbalimbali kama vile za Dawasa, Luku na malipo ya serikali.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa kutangaza kugawa faida hiyo, Mkurugenzi wa Airtel Money, Isack Nchunda, alisema: "Faida itokanayo na matumizi ya Airtel Money itagawiwa kwa wateja wa Airtel Money na mawakala wote nchini ambao wametumia huduma ya Airtel Money kwa miezi 12 iliyopita kati ya Aprili na Septemba, 2019.

"Airtel inaendelea kuunga mkono juhudi za serikali zinazochochea kusambaa na upatikanaji wa huduma za kifedha nchini kwa kutoa faida kila robo ya mwaka. faida hii itawawezesha wateja kupata Sh. bilioni 2.6 zitakazokwenda kwa wateja na mawakala waliotumia huduma kwa kipindi hicho.

"Tunayo furaha kuona ukuaji mzuri kwenye huduma ya Airtel Money kwani mpaka sasa huduma zetu zimekuwa zikikuwa mfululizo kwa ukuaji wa tarakimu mbili," alisema Nchunda.

"Kuanzia leo wateja wote wa Airtel Money wataweza kutumia fedha zao za faida kwa kununua LUKU, kununua muda wa maongezi au bando au kwa matumizi yoyote yale," alisema Nchunda.

Mkurugenzi huyo alisema Airtel Tanzania imedhamiria kuendelea kuboresha na kupeleka karibu huduma za Airtel Money ili kufikia maelfu ya Watanzania ambao bado hawajafikiwa na huduma za kibenki na hasa maeneo ya vijijini.

Katika kufanikisha hilo, alisema hivi karibuni Airtel ilizindua kampeni ya 'Tuko Nawe Kila Kona' kwa lengo la kuimarisha huduma ya maduka ya 'Airtel Money Branches' ambayo ni moja ya mikakati muhimu ya kusambaza huduma ya Airtel Money nchini.

Pia alisema Airtel imezindua bando za 'Dabo Data Smatika' kupitia Airtel Money kwa lengo la kuongeza huduma kwenye huduma zinazotolewa na Airtel Money katika zaidi ya matawi 1,000 nchini.

Naye Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel Tanzania, Beatrice Singano, alisema lengo la kampuni ni kuendelea kuwafikia wateja ambao ni muhimu kwenye biashara.

"Tunaendelea na uzinduzi wa maduka ya Airtel Money Branches ili kuhakikisha kuwa na huduma za kifedha za Airtel Money zinaendea kupanuka na kuwafikia wateja wengi kuliko huduma yoyote ya kifedha nchini. Wateja wetu tunawahakikishia huduma za papo kwa hapo za kutoa pesa ni bure," alisema.




Waumini wa Kanisa Katoliki Parokia ya Kimara Mavurunza, wakinawa mikono kabla ya kuingia kwenye Misa ya mazishi ya aliyewahi kuwa mwandishi wa gazeti la Nipashe, Oswald Rutahiwa, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Afariki dunia tukio wizi pikipiki

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKAZI wa Kijiji cha Ninga, Kalambo mkoani Rukwa, Steven Kalunga (29), amefariki dunia katika kijiji cha Miangalua wilayani Sumbawanga wakati akiwa katika jaribio la kuiba pikipiki na fedha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Justin Masejo, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Machi 17, mwaka huu, majira ya saa 2:30 usiku kijijini hapo.

Kamanda Masejo alisema siku ya tukio hilo, Kalunga akiwa na mwenzake ambaye jina lake halikufahamika mara moja, walitega waya ngumu barabarani na kusababisha Joseph Kachingwe aliyakuwa akiendesha pikipiki kupata ajali kwa kuanguka kutokana na mtego huo.

Baada ya mwendesha pikipiki huyo kuumia, alisema Kalunga na mwenzake huyo walimvamia na kumpora Sh. milioni 1.5 na pikipiki yake yenye namba za usajili MC 617 CCG na kuipanda kisha kukimbia nayo.

Alisema Kachingwe alifanikiwa kuinuka na kupiga kelele kuomba msaada ndipo kundi la watu walipojitokeza kwa lengo la kumsaidia na walianza kuwafukuza watuhumiwa na kutokana na kuwa katika mwendokasi mkubwa walipata ajali na kuanguka.

Katika ajali hiyo, Kalunga aliumia vibaya ndipo walipomkamata na kumkimbiza Kituo cha Afya cha Laela, lakini alifariki dunia wakati akiendelea na matibabu, huku mtuhumiwa mwingine alifanikiwa kukimbia na fedha ambazo waliziiba.

Kamanda Masejo alisema kuwa juhudi za kumtafuta mtuhumiwa aliyekimbia bado zinaendelea ili afikishwe mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

# Walia ukosefu vitakasa mikono

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Wafanyabiashara Mkoa wa Pwani, Abdallah Ndauka, ameomba mamlaka zinazohusika kuweka maji tiba kwenye stendi ya mabasi ya Maili Moja ili kuwezesha wananchi kujikinga na virusi vya corona.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ndauka alisema kama uwezo wa kununua vitakasa mikono na kama hawana waweke hata ndoo ya maji ili wanaoingia katika stendi hiyo wapate huduma ya kunawa mikono.

Alisema nchi zingine wamewajibika ipasavyo na kusababisha kupunguza maambukizi, hivyo hata hapa nchini inatakiwa mamlaka zinazohusika kuwajibika ipasavyo.

Pia alisema elimu inatakiwa kutolewa kwa wananchi kutambua namna ya kujikinga na vifaa vinavyotakiwa kutumika ili kuepuka maambukizi ya ugonjwa huo.

Ramadhani Mkabala, mkazi wa Maili Moja, alisema wako watu wanaotembeza vifaa vya kujikinga na virusi vya corona, hivyo washirikiane na mamlaka zinazohusika kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea endapo havitakaguliwa.

"Watu wengi sasa wanapita mitaani wanauza maji tiba lakini hatujui kama ndivyo vyenyewe vinavyotakiwa. Elimu ifike mpaka huku chini wananchi wajue vifaa sahihi vinavyotakiwa maana badala ya kujikinga tunaweza kuongeza madhara zaidi," alisema.

Nipashe ilitembelea baadhi ya maduka ya dawa za binadamu na kubaini kukosekana kwa maji tiba huku maduka mengine vitakasa mikono vikiuzwa Sh. 35,000 badala ya Sh. 10,000 kabla ya ugonjwa huo kuingia nchini.

Baadhi ya wauzaji wa maduka hayo walisema vifaa hivyo vinauliziwa na wananchi wengi lakini upatikanaji wake ni wa shida.

**Nchi zingine wamewajibika ipasavyo na kusababisha kupunguza maambukizi, hivyo hata hapa nchini inatakiwa mamlaka zinazohusika kuwajibika ipasavyo.**

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**VIWANJA VINAUZWA,** Headline block ya viwanja vine inauzwa, Viko mbweni mpiji karibu na Shule ya Sekondari Mpiji . Eneo zaidi ya heka moja ) 4220 Sq mt . Viwanja Surveyed. Simu: 0711 506758 0787 445506, 0679 041220


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


## KUPOTEA KWA CHETI



**Petro Masero Mwita** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index **P.136/19**, Kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1983 katika Shule ya Sekondari Musoma . Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **TAR/IR/159/87**

115673302

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FATUMA SHARIFF JUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 751 AFE MITSUBISHI FUSO**. Chassis namba **FK417K544432.** Engine namba **6D15659474.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/127444/2020.**

115673502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RASHID KHATIBU MADOTI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 353 AGR MITSUBISHI CANTER.** Chassis namba **FE435EV51425.** Engine namba **4D34H27344.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/RB/233241/2020.**

115673602

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI NO.325/2018**

**GEORGE GODWIN SANGA::::::::::::::::MDAI**
**Versus**
**NMB PLC MWANJELWA BRANCH:::::MDAIWA WA KWANZA**
**BURTON S MAHENGE:::::::::::::::::::MDAIWA WA PILI**
**JANE R KAMETA::::::::::::::::::::::::::MDAIWA WA TATU**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA: 1.BURTON SIMON MAHENGE**
**2.JANE RUBEN KAMETA**

Fahamu kwamba amefungua shauri dhidi yenu katika baraza hili. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 31/03/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masjala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.

Kumbuka:Usipohudhuria siku hiyo Baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 06/03/2020.

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**

**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU WILAYA YA GEIT**

**SHAURI LA MADAI NA: 12/2020**

**MDAI: DOTTO SOSPETER NDEGE**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: ANNA NYAKWESI MKAMA**

**POPOTE ALIPO TANZANIA BARA NA VISIWANI**

**AMRI:**
Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 20/3/2020 saa 2:30 Asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo ALHAMISI tarehe 12 mwezi MARCH, 2020.


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# BAYERN WAFANYA MAZUNGUMZO YA SIRI NA SANE

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Bayern Munich imeripotiwa kwamba imefanya mazungumzo ya siri na wakala wa winga wa Manchester City, Leroy Sane ili kumsajili kipindi cha majira ya joto kinachokuja.

Mazungumzo hayo yalifanyika kati ya Mkurugenzi wa Michezo wa Bayern, Hasan Salihamidzic na wawakilishi wa Sane kampuni ya LIAN Sports wiki iliyopita, kwa mujibu wa gazeti la michezo la Ujerumani, Bild.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 amekuwa akiwaniwa zaidi na Salihamidzic ambaye ameripotiwa kufanya mazungumzo na wakala wa mchezaji huyo mara kadhaa.

Gazeti la Bild limeripoti kwamba, Fali Ramadani, mmoja wa washauri wa wachezaji wenye ushawishi mkubwa Ulaya na Mkurugenzi wake mkuu Damir Smoljan ambaye alimwingiza Sane kwenye Kampuni ya LIAN, alisafiri kwenda Munich kwa ajili ya mazungumzo hayo.

Sane aliondoka kwenye kampuni ya wakala ya David Beckham, DB Ventures Limited na kujiunga na kampuni ya LIAN, Januari, lakini washauri wake wapya watakuwa na uwezo wa kuingia kwenye mazungumzo rasmi Aprili Mosi mwaka huu.

Mkataba wa mchezaji huyo raia wa Ujerumani pale kwenye dimba la Etihad unamalizika mwakani, lakini Munich wanaandaa ofa nene kwa ajili ya kumtwaa nyota huyo.

Winga huyo alionekana kama angehamia pale kwenye dimba la Allianz Arena kipindi cha majira ya joto kilichopita, lakini kuumia goti wakati wa mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Liverpool Agosti mwaka jana kulitibua dili hilo.

# Smalling bado hajaamua hatima yake

**ROME,** Italia

CHRIS Smalling bado hajaanza majadiliano ya wapi atakwenda na atafanya maamuzi wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Mlinzi huyo wa kati wa Manchester United amekuwa na wakati wa kuvutia pale AS Roma anakocheza kwa mkopo na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kuitwa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England.

Kiwango chake pia kimeifanya Roma kuonyesha nia ya kutaka kumpa mkataba wa kudumu, huku Arsenal, Everton, Leicester na Tottenham pia zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili England.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 bado hajapewa ofa kutoka klabu yoyote, huku mwenyewe akisisitiza anataka kwanza kumaliza msimu kule Italia.

Smalling, ambaye amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake na United ana kipengele cha kuongeza mwaka mmoja pale Old Trafford ikitegemea mazungumzo na Ole Gunnar Solskjaer kipindi cha majira ya joto.

Hata hivyo, beki huyo mzaliwa wa Greenwich na mkewe Sam wameonyesha kuwa wanafurahia zaidi maisha yao nchini Italia na amekuwa akipendwa zaidi na mashabiki wa Roma.







# Beki wa Brazil kumrithi Pique

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamechagua mlinzi wa Lazio, Luiz Felipe raia wa Brazil kwa ajili ya kumsajili kipindi cha majira ya joto.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 anatazamwa kama mrithi wa muda mrefu wa mlinzi wa kati wa miamba hao wa Katalunya, Gerard Pique ambaye alifikisha umri wa miaka 33 Februari.

Kwa mujibu wa gazeti la nchini Hispania la Mundo Deportivo, ofa ya pauni milioni 18 kutoka Barcelona inaweza kutosha kumsajili Luiz, ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022.

Klabu hiyo ya Katalunya wanamwona mlinzi huyo kama chaguo sahihi la kuwa mrithi wa gwiji Pique, ambaye amecheza mechi 531 kwa Barcelona tangu alipoanza kuichezea mwaka 2008.

Barcelona kwa sasa wana walinzi wa kati, Clement Lenglet na Samuel Umtiti, huku pia Junior Firpo anaweza kucheza katikati.

## HABARI MICHEZO

# Kepa yupo tayari kugombea namba Chelsea

**LONDON,** England

GOLIKIPA wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga anataka kubaki na kupigania majaliwa yake hapo Stamford Bridge na anaamini ana sapoti kutoka kutoka kwa klabu hiyo.

Licha ya kumsajili kwa pauni milioni 71.6 kutoka Athletic Bilbao, lakini umuhimu wake umeonekana mdogo msimu huu na Kocha Frank Lampard amemwonya Kepa kwamba anatakiwa kujituma zaidi ili kupata nafasi ya kucheza.

Ingawa alirudi kwenye nafasi ya kuanza na kusifiwa kwa kiwango chake, Chelsea inaangalia uwezekano wa kuongeza golikipa mwingine kipindi cha usajili wa majira ya joto, ambapo kipa mwingine, Willy Caballero atatimiza umri wa miaka 39 Septemba mwaka huu.

Kipa wa Manchester United, Dean Henderson, Juan Musso wa Udinese, Andre Onana wa Ajax na Gianluigi Donnarumma wa AC Milan wametajwa kuwaniwa na Chelsea.

Hata hivyo, Kepa mwenye umri wa miaka 25 amebainisha kuwa na furaha na maisha ya pale jiji la London na amehakikishiwa na maofisa wakubwa kwamba ataendelea kuwapo hapo hata kama Lampard anataka kuleta ushindani wa makipa wapya.






# UNITED YAJIANDAA KUACHANA NA POGBA

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imeripotiwa ipo tayari kumalizana na Paul Pogba wakiwa wanajiandaa kutokuwa na mshambuliaji aliyeweka rekodi ya usajili wakati akitua hapo Old Trafford.

Na sasa wapo tayari kusikiliza ofa ya kiwango walichokiweka ya pauni milioni 100 kwa ajili ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto kinachokuja, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Majaliwa ya Pogba pale Old Trafford yamekuwa shakani kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita baada ya kushindwa kukamilisha uhamisho wa kwenda Real Madrid kipindi cha majira ya joto kilichopita.

United walikuwa wanataka kulipwa pauni milioni 150 ili kumuuza mchezaji huyo mwaka 2019, lakini sasa watalazimika kupunguza bei licha ya kuwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja kwenye mkataba wake.

Wote mchezaji na klabu tayari wamekubaliana kuachana, licha ya kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer kuanza kurudi kwenye kiwango chake.

Pogba ambaye kwa sasa anapambana kupona kutoka majeruhi, amecheza mechi mbili tu tangu Septemba mwaka jana.

Alitarajiwa kurudi uuwanjani mwezi huu baada ya kufanyiwa operesheni ya kifundo cha mguu, lakini ligi sasa imesimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

# *Coutinho anukia Stamford Bridge*

**BARCELONA,** Hispania

CHELSEA inaongoza kwenye mbio za kumsajili Philippe Coutinho, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Bayern Munich akitokea Barcelona.

Mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool, ambaye alikuwa pale kwenye dimba la Anfield kuanzia mwaka 2013 hadi 2018, na alisajiliwa kwa kitita kikubwa cha fedha kwenda Barca Januari 2018, lakini akakutana na wakati mgumu wa kushindwa kuonyesha kiwango alichokuwa nacho kule kwenye Ligi Kuu England kwa kipindi cha miezi 18 aliyokaa pale Nou Camp.

Akakosa namba Barca chini ya kocha, Ernesto Valverde ambaye alimpeleka Bayern, lakini sasa anaonekana anaweza kurudi England, huku Chelsea ikiwa na nafasi kubwa ya kumsajili, kwa mujibu wa gazeti la Hispania la AS.

Ripoti zinasema kwamba, Chelsea wameshawasiliana na klabu ya Coutinho, Barca na mchezaji mwenyewe ameonyesha nia ya kutaka kurudi katika Ligi Kuu England.

Huku winga Willian mkataba wake ukiwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, kocha wa Blues hao, Frank Lampard anaonekana anataka kusajili wachezaji wapya kwenye eneo la ushambuliaji.

Na huku ikionekana wazi kwamba Coutinho hawezi kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Barca msimu ujao chini ya kocha mpya Quique Setien, ana nafasi kubwa ya kutua pale Chelsea.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amecheza mechi 22 kwa miamba hao wa Ujerumani, huku akifunga mabao nane na alianza katika mechi 15.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# UNITED, MAN CITY ZAMWANIA NIGUEZ

●●● Ni baada ya kiungo huyo kukataa kusaini mkataba mpya na Atletico ambao wamegoma...

**MADRID,** Hispania

MAHASIMU wa jiji la Manchester, klabu za Manchester United na Manchester City zimetajwa ziko katika mipango ya kupambana kuwania saini ya kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez katika majira ya joto.

**City na United zimeingia vitani kuwania saini ya Niguez baada ya kiungo huyo kutofikia makubaliano na klabu yake ya kusaini mkataba mpya.**

Klabu hizo mbili za Manchester zimekuwa zikivutiwa na nyota huyo wa Atletico kwa muda mrefu, ambaye thamani yake iliyotajwa katika mkataba ni pauni milioni 141 na hivi karibuni aliisaidia timu yake kuiondoa Liverpool katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Niguez alifunga bao pekee katika mechi ya kwanza ya hatua ya 16 bora lililowaondoa Liverpool katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano.

Mkataba wa sasa wa kiungo huyo unatarajiwa kumalizika katika kipindi cha majira ya joto mwakani na mazungumzo na klabu yake yameshindwa kufikia muafaka kutokana na kipengele cha malipo ya mshahara, vyombo vya habari mbalimbali vya Hispania vimeandika.

Baada ya Antoine Griezmann kuondoka Atletico na kujinga na Barcelona mwaka jana, klabu hiyo iliamua kupunguza mishahara ya wachezaji wake waliobakia, uamuzi ambao uliwafanya nyota waliobakia kutokuwa na furaha akiwamo Niguez, gazeti la Mundo Deportivo liliandika.

Gazeti hilo likaendelea kuandika kuwa Saul Niguez naye hakuwa na furaha na mabadiliko hayo ya mshahara yaliyofanywa na mabosi wao.

Nyota huyo anawakilishwa na Kampuni iitwayo Stellar, inayosimamiwa na wakala wa Gareth Bale, Jonathan Barnett, na Mundo liliendelea kuandika kuwa hali hii itapelekea mchezaji huyo kufanya mchakato wa kujiunga na Ligi Kuu England.

Mazungumzo na Atletico yalisimama kwa zaidi ya mwezi bila ya kupata ufumbuzi, na hiyo inamfanya kiungo huyo mwenye umri wa miaka 25 anayeichezea Timu ya Taifa ya Hispania kukaribia kujiunga na moja ya klabu hizo za jijini Manchester.

Niguez alibakia kuwa mmoja wa wachezaji muhimu katika kikosi cha Diego Simeone, pamoja na Koke na Jan Oblak, na kitendo cha kumpoteza nyota huyo wa zamani aliyekulia kwenye kituo chao kinaweza kuwa janga kubwa kwa Atletico.

United iko katika mchakato wa kusaka viungo mahiri, huku hatima ya kuendelea kubakia klabuni Paul Pogba ikionekana kufikia mwisho wakati City yenyewe inasaka nyota atakayeziba pengo la Fernandinho.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL, CHELSEA VITANI

ARSENAL na Chelsea zote zimeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Bayer Leverkusen na Timu ya Taifa ya Jamaica, Leon Bailey (22), ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 85. ***(Daily Express)***

### AUBAMEYANG SAFARI IMEIVA

ARSENAL imekubali kumpoteza straika wake Pierre-Emerick Aubameyang (30), katika majira ya joto na inahitaji kulipwa pauni milioni 55 na klabu inayomhitaji huku tayari Barcelona ikionyesha nia ya kumsajili nyota huyo wa Timu ya Taifa ya Gabon. ***(Sport, in Spanish)***

### JUDE ANUKIA DORTMUND

BORUSSIA Dortmund iko mbele dhidi ya Liverpool, Manchester United na Chelsea katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 ya England (U-17), Jude Bellingham (16), anayechezea Birmingham. ***(Bild, in German)***

### CITY, JUVE, PSG VITANI

MANCHESTER City, Juventus na Paris St-Germain zimeonyesha nia kuwania saini ya kiungo wa Lyon Mfaransa Houssem Aouar ambaye ana umri wa miaka 21. ***(Corriere dello Sport, in Italian)***

### ROBACK AINGIA SOKONI

ARSENAL inaendelea na mazungumzo na Hammarby kwa ajili ya kunasa saini ya mshambuliaji chipukizi raia wa Sweden, Emil Roback (16), ambaye anaivutia klabu ya Bayern Munich. ***(Daily Mail)***

### SANDERSON ATAJWA WEST

WEST Ham imeanza mchakato wa kuwania saini ya beki raia wa England, Dion Sanderson (20) ambaye yuko kwa mkopo katika klabu ya Cardiff akitokea Wolves. ***(Daily Mail)***

### COUTINHO KUTUA CHELSEA

CHELSEA imefanya mazungumzo na Barcelona kuhusiana na uwezekano wa kumsajili kwa mkopo kiungo wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho (27), katika msimu ujao. ***(Sport, in Spanish)***

### CAZORLA KUREJEA ARSENAL

ARSENAL imeanza mazungumzo na kiungo wa Villarreal, Santi Cazorla ili kumsajili katika majira ya joto kwa lengo la kumpa nafasi Mhispania huyo mwenye umri wa miaka 35 kuaga mashabiki wake wa Gunners baada ya kuihama klabu hiyo mwaka 2018, lakini akashindwa kucheza kutokana na kuwa majeruhi kwa muda wa miaka miwili. ***(Daily Express)***

### YOUNG MAMBO SAFI

INTER Milan inajiandaa kumpa mkataba wa mwaka mmoja beki raia wa England, Ashley Young (34), baada ya kuonyesha kiwango kizuri tangu alipotua katika klabu hiyo Januari mwaka huu akitokea Manchester United. ***(Gazzetta dello Sport, in Italian)***

### O'NEIL KUBAKIA IRELAND

CHAMA cha Soka cha Ireland kimesema kinamtaka Kocha wa Stoke City, Michael O'Neill kuendelea kuifundisha timu yake ya Taifa katika mechi za mtoano za kuwania tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Euro 2020, ambazo zimesogezwa mbele hadi Juni kwa sababu ya kuwapo kwa maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona. ***(Daily Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Riadha wajifua kama kawaida

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya riadha ya mkoa wa Dar es Salaam inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Taifa yanayotarajiwa kufanyika mapema Mei mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Idd Muhunzi alisema wachezaji wake wanaendelea na programu ya mazoezi ili kujiweka tayari na mashindano hayo, lakini wakijilinda na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19).

"Tunaendelea na mazoezi huku tukiwa na tahadhari ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, ugonjwa ambao umevunja na kusimamisha shughuli nyingi," alisema Muhunzi.

Alisema wameshindwa kusimamisha mazoezi kutokana na aina ya mchezo wanaoshiriki na endapo wangeahirisha, uwezekano wa kufanya vibaya ungekuwa mkubwa.

"Nafahamu wachezaji wangu wakikaa kwa muda mrefu bila kufanya mazoezi wataharibu kila kitu kwenye mashindano, miili yao ingepoa," Muhunzi alisema.

Aliongeza mbali na mazoezi ya viungo, wachezaji wake pia wanapata elimu ya kisaikolojia ili kuwaweka imara kila idara na hatimaye kufanya vema katika michuano hiyo.

## Coastal Union hakuna kulala

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, amesema wachezaji wake wataendelea kujifua kwa kufuata programu maalumu ya mazoezi aliyowapa ili kuwaimarisha kufuatia mechi za Ligi Kuu Bara kusimama ili kujiepusha na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), imeelezwa.

Mgunda aliliambia gazeti hili kuwa amewapa majukumu wachezaji wake na watatakiwa kutekeleza maelezo hayo.

"Licha ya kutokuwa na mazoezi ya pamoja, kila mchezaji ataendelea na mazoezi binafsi, nimewapa majukumu na programu ambazo kila mmoja atazifanya akiwa nyumbani ili tukirudi wote viwango viwe sawa," alisema Mgunda.

Alisema Coastal Union inaungana na agizo la serikali la kukataza mkusanyiko.

"Serikali imekataza mkusanyiko wa watu hii ni kwa ajili ya kutulinda wananchi wake, hivyo lazima na sisi tukiri na kufuata maagizo kwa sababu hili janga ni la dunia," alisema Mgunda.

Hadi Ligi Kuu inasimama, Coastal Union iliyocheza mechi 28, imejikusanyia pointi 46 na katika msimamo iko kwenye nafasi ya tano.



# GWAMBINA, MBAO FC ZAENDELEA KUJIIMARISHA

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI baadhi ya timu zikivunja kambi kwa muda wa siku 30 ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, klabu za Gwambina FC na Mbao FC zimesema wachezaji wao wataendelea na programu za mazoezi kama kawaida.

**Gwambina FC inaongoza katika msimamo wa Kundi B ikiwa na pointi 40 katika Ligi Daraja la Kwanza inapambana kupanda daraja wakati Mbao FC inayoshiriki Ligi Kuu Bara yenyewe inahitaji kujinusuru na janga la kushuka daraja.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Gwambina, Fulgence Novatus alisema bodi ya timu hiyo imeamua timu yao isivunje kambi na iendelee na mazoezi kwa ajili ya kujiimarisha katika 'vita' ya kupanda daraja waliyonayo.

Novatus alisema kikosi kilitarajia kurejea jijini Mwanza jana baada ya mchezo wao dhidi ya Transit Camp ya Dar es Salaam uliotarajiwa kuchezwa Jumamosi iliyopita kuahirishwa kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona.

"Gwambina hatutavunja kambi, tunaendelea kujifua kwa ajili ya kukiimarisha kikosi changu, kwa ajili ya mechi za lala salama, pia tulikuwa na wachezaji majeruhi ambao wamerejea kundini ili kuwafanya wawe fiti, tumedhamiria kupanda daraja msimu huu, " alisema Novatus.

Wakati huo huo Mbao FC nayo imesema itaendelea na kambi licha ya serikali kusimamisha mechi za Ligi Kuu kutokana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, imefahamika.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Agustino Malindi alisema kikosi chake kitaendelea na mazoezi, lakini wakiwapa wachezaji elimu maalum kuhusiana na kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huo.

"Tutaendelea na kambi tukiwa na tahadhari kubwa ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona, tuko katika hali mbaya, tunahofia kushuka daraja," alisema kwa kifupi kocha huyo.

Aliongeza wameamua kutovunja kambi yao kutokana na maendeleo ya timu kutokuwa mazuri na wanahitaji kujiokoa na janga la kushuka daraja.

Alieleza hofu ya kuwapo kwa corona imemuharibia utaratibu wake wa kuwajenga wachezaji ambapo alitumia nguvu nyingi kujiandaa na michezo iliyokuwa mbele yao.




Wachezaji wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi ya kusaka tiketi ya kufuzu mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika dhidi ya Tunisia na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo zimeahirishwa kutokana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19). **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Ligi Kuu Zanzibar yasimama rasmi*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza kusimamisha ligi zake zote kutokana na tamko lililotolewa na serikali kupitia Wizara ya Afya ili kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), ambao umeingia nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa ZFF, Mohamed Ali Hilali, ilisema ligi hizo zimesimamishwa kwa muda usiojulikana mpaka pale serikali itakapotoa tamko lingine kuhusiana na kuendelea kwa shughuli mbalimbali za kila siku.

Hilali alisema kwa hivi sasa tayari shirikisho hilo lishatoa barua kwa mikoa iwaharifu ngazi za wilaya juu ya kusitisha shughuli zote za michezo mpaka pale litakapotoka tamko lingine la serikali ambalo litaruhusu kufanya hivyo.

Kiongozi huyo amevitaka vilabu pamoja na wanamichezo wote kufuata maelekezo yanayotolewa na Wizara ya Afya kuhusiana na taratibu za kujikinga na virusi vya ugonjwa huo ambavyo vinaenea kwa kasi ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

"Tunatangaza kusimamisha rasmi ligi zetu zote ambazo zinasimamiwa na ZFF, hii inatokana na kutii tamko la serikali, lakini tunatarajia kuwa na kikao cha Bodi ya Ligi ili kupanga maazimio mengine yatakayotoa mustakabali wa ligi zetu," alisema Hilali.

Alieleza baadhi ya ligi zilikuwa zinaelekea ukingoni na kikao cha bodi hiyo kitatoa mwongozo wa hatima ya mechi zilizobakia.

Hadi Ligi Kuu Zanzibar inasimamishwa rasmi hapo juzi, timu ya KMKM yenye pointi 44 ndiyo ilikuwa inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa kisiwa hicho kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Michezo

Ijumaa Machi 20, 2020

Nipashe




United, City zamwania Niguez UKURASA 30



Kiungo wa Yanga, Haruna Niyonzima (kushoto), akijipanga kuondoka na mpira huku mchezaji wa KMC, Hassan Kabunda akijaribu kumdhibiti katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa hivi karibuni kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. Yanga ilifungwa bao 1-0. **PICHA : JUMANNE JUMA**

## Yanga yajipanga kurejea kivingine

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI kikosi cha Yanga kikiwa kwenye mapumziko ya muda kufuatia kuwapo kwa maambukizi wa virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), uongozi wa klabu hiyo umepanga utarejea na nguvu mpya baada ya tamko la kusimamisha mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara litakapomalizika.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, ameliambia gazeti hili kuwa kambi za timu hiyo ambayo iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara imevunjwa, lakini benchi la ufundi limewapatia programu maalumu wachezaji wao ili kuwajenga.

Bumbuli alisema wanaamini wachezaji wao wakiwa na nidhamu nzuri kwa kufuata programu waliyopewa, watarejea wakiwa imara na kufanya vema katika mechi zitakazofuata.

"Mwalimu ametoa programu maalumu, yaani programu ya mtu mmoja mmoja, mchezaji binafsi atatakiwa kufanya mazoezi akiwa nyumbani kutokana na nafasi ya kujifua pamoja kusimama, mpaka hapo tutakavyotangaziwa vingine na serikali, ila tutawafuatilia ili kujua maendeleo yao," Bumbuli alisema.

Alisema kambi nyingine walizovunja ni ya timu ya vijana ya umri chini ya miaka 17 na ile ya wanawake (Yanga Princess), ambazo ligi zao pia zimesimamishwa.

Tangu Yanga ilipowafunga watani zao Simba katika mechi iliyochezwa Machi 8, mwaka huu, timu hiyo iliyoko chini ya Mbelgiji Luc Eymael imeambulia pointi moja kwenye mechi mbili ilizocheza.

# Simba, Yanga zaigomea TFF

**Na Somoe Ng'itu**

### ●●● Ni uamuzi wa kucheza ligi bila mashabiki, zaeleza shirikisho limefanya haraka na kushauri kusubiri...

UAMUZI wa kutangaza uwezekano wa kucheza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara bila ya kuhudhuriwa na mashabiki umeelezwa kutolewa kwa haraka kabla ya kusubiri taarifa za maendeleo ya kuhusiana na hali ya maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19), ambayo yameingia nchini.

**Ikiwa imepita siku moja baada ya serikali kusimamisha shughuli mbalimbali za mikusanyiko, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kupitia Kamati ya Bodi ya Ligi Nchini (TPLB), lilitangaza juzi mechi za Ligi Kuu Bara zinaweza kuendelea lakini bila ya mashabiki ili kukamilisha msimu wa 2019/2020.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Crescentius Magori, alisema uamuzi huo ulitolewa kwa makosa na Bodi ya Ligi ilipaswa kusubiri kupokea taarifa kuhusiana na hali ya maambukizi baada ya kupita wiki mbili au tatu.

Magori alisema kutangaza kuendelea na mechi za ligi mbalimbali bila mashabiki kwa sasa haikuwa sahihi kwa sababu huenda hali ya maambukizi inaweza kuwa mbaya zaidi na hivyo kuathiri wachezaji na viongozi watakaosimamia michezo hiyo.

"Ni uamuzi wa haraka, huwezi kujua huko mbele hali itakuwaje, huenda ikadhibitiwa mapema na hali ikarejea sawa sawa au hali ikawa mbaya zaidi hata kuchezwa bila mashabiki haiwezekani, nashauri tathmini ingefanyika kuanzia wiki ya tatu baada ya tamko la kusimamisha ligi," alisema Magori.

Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, aliliambia gazeti hili uamuzi huo uliotangazwa na Bodi ya Ligi si sahihi na si suluhisho kwa tishio lililopo la ugonjwa huo ambao unaisumbua dunia kwa sasa.

Mwakalebela alisema TFF na vyombo vyake inapaswa kuwa na subira kwa sababu endapo virusi vya corona vitaendelea kuwapo, itakuwa vigumu kudhibiti mkusanyiko wa mashabiki kwenye 'vibanda umiza' ambavyo vimeenea katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

"Bado haitakuwa suluhisho, mkusanyiko wa watu utaendelea kuwapo, hatuna uwezo wa kudhibiti katika maeneo mbalimbali nchini ambayo yatakusanya mashabiki, ni bora tusubiri janga limalizike, huko duniani (nchi zilizoendelea), wameona haina tija, iweje sisi tucheze," Mwakalebela alisema.

Naye mchambuzi maarufu wa soka na nyota wa zamani wa Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), Ally Mayayi alisema mechi za Ligi Kuu Bara kuchezwa bila mashabiki zitakuwa na madhara kiuchumi kwa klabu zote zinazoshiriki ligi hiyo.

Mayayi alisema klabu zote zinategemea kujiendesha kwa kutegemea mapato ya milangoni, hivyo kuchukua uamuzi huo kutazifanya timu kuyumba.

"Kwanza ligi kusimama kwa siku 30 kuna madhara makubwa sana, kutafanya viwango vya wachezaji kushuka, upo uwezekano mkubwa wachezaji wakarejea wakiwa hawako fiti, hii italeta matatizo na kuzalisha matokeo yasiyotarajiwa," alisema Mayayi.

Aliongeza kusimama kwa ligi kutazalisha madeni ambayo klabu hazikujiandaa kutokana na kuzuka kwa janga hilo ambalo limesimamisha ligi na mashindano mbalimbali duniani.

"Hata bajeti zilizopo kwa klabu imekuwa haitoshi, ligi itakapokuwa imesimama ni wazi kutakuwa na gharama ambazo zitakuwapo, kuna klabu zimekuwa zinapata tabu hata ya usafiri na malazi, klabu zitazalisha madeni mapya, malimbikizo ya posho kama ambayo tumekuwa tukisikia malalamiko ya kudai mishahara," Mayayi aliongeza.

Simba ndio mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu wakiwa wamejikusanyia pointi 71 wakifuatiwa na Azam FC yenye pointi 54 na Yanga yenye pointi 51, lakini imecheza mchezo mmoja pungufu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042